



**Muhimbili** watoa ushanga katika mapafu ya mtoto

UKURASA 2



**Mawaziri** Tanzania, Kenya waingilia kati zuio la ndege

UKURASA 4



**Mgambo** wadaiwa kupiga, kumwagia maji vitanda vya wasiolipa kodi

UKURASA 16

**MESSI ATWAA TUZO YA FIFA**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatano Januari 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581558

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US www.twitter.com/nipashetz

www.ippmedia.com www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


## MTIHANI WAVUJA

# Wauguzi 1,330 wafutiwa matokeo



• **Anayedaiwa** kuvujisha aingia matatani... *Endelea ukurasa 2*







Meli kubwa ya Norwegian Cruise Line (NCL) iliyobeba watalii 2,210 na wahudumu 1,011 yenye urefu wa mita 294 ikiwa imetia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam jana ikitokea Mombasa nchini Kenya. Picha ndogo: Baadhi ya watalii wakishuka bandarini hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Meli kubwa yenye watalii 2,200 yatia nanga Dar

UKURASA 8

# Shule 'yamchokoza' waziri

• **Yatoza** michango iliyopigwa marufuku... *Endelea ukurasa 3*

**MICHEZO** TAIFA STARS YASAKA REKODI AFCON LEO UK.24

**KATUNI** UK.6

# Wauguzi 1,330 wafutiwa matokeo ya mtihani

**Na Beatrice Shayo**

WAHITIMU 1,330 wenye elimu ngazi ya stashahada katika uuguzi na ukunga, wamefutiwa matokeo ya mtihani wa usajili na leseni ya Baraza la Uuguzi na Ukunga baada ya kuvuja.

Wakati wauguzi na wakunga hao wakifutiwa matokeo hayo, Wizara ya Afya imetangaza kumsimamisha kazi anayetuhumiwa kuvujisha mtihani huo.

Kuvuja kwa mitihani ni mfupa mgumu kwa kuwa Novemba 5, 2021, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTEVET) ilifuta matokeo yote ya mitihani ya nadharia ya programu ya utabibu ngazi ya Stashahada (NTA 5) kwa vyuo vyote nchini baada ya kuthibitika kuvuja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Afya, Englibert Kayombo, wahitimu hao watapewa nafasi ya kufanya mtihani mwingine bila malipo Februari 16, mwaka huu mkoani Dodoma.

Alisema taarifa zaidi kuhusu kurudiwa kwa mtihani huo zitatolewa na baraza, hivyo watahiniwa wote wanatakiwa kujiandaa kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria.

"Hatua hizi zimechukuliwa kwa lengo la kuhakikisha baraza linathibitisha wataalamu wenye sifa stahiki kulingana na taaluma zao kutoa huduma bora za matibabu kwa wagonjwa na kuzingatia usalama wa mteja anayetegemea kupata huduma za uuguzi na ukunga. "Hii ni kwa mujibu wa sheria ya uuguzi na ukunga ya mwaka 2010 ambalo ndilo jukumu kubwa la baraza," ilisema taarifa hiyo.

Pia alisema Baraza la Ukunga na Uuguzi Tanzania chini ya Wizara ya Afya lina jukumu kusimamia taaluma za wauguzi na wakunga nchini kupitia Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Pamoja na majukumu mengine ya msingi, alisema baraza limepewa jukumu la kusajili, kuorodhesha na kutoa leseni kwa wauguzi na wakunga ya ngazi zote kwa kuendesha mitihani ya usajili na leseni kwa mujibu wa kifungu cha 15(a) (b) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

"Septemba 7, mwaka jana, baraza liliendesha mitihani ya usajili na leseni kwa wauguzi na wakunga 1,434 wa ngazi zote. Watahiniwa wa astashahada walikuwa 44, stashahada 1,330, shahada 60.

Kayombo alisema kuwa mitihani hiyo ilifanyika katika vituo vitatu kwenye mikoa ya Dar es Salaam (Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam- DUCE), Mwanza (Chuo Kikuu Mwanza) na Dodoma (Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana- SJUIT).

Alisema wizara ilipata taarifa za kuvuja kwa mitihani na kuchukua hatua za haraka kushirikiana na vyombo vya usalama kufanya uchunguzi na kuthibitika kuwa ni kweli mtihani ulivuja na kusambaa kwa watahiniwa wa stashahada.

Pia alisema mtuhumiwa aliyehusika katika uvujishaji wa mtihani huo tayari amebainika na kusimamishwa kazi huku taratibu za kinidhamu na kisheria zinaendelea kutekelezwa.



Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri katika Ikulu Tunguu, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Tanzania, Angola kushirikiana sekta za afya, mafuta na gesi

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na Serikali ya Jamhuri ya Angola zimetia saini hati tatu za makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi, kuondoleana visa kwa wenye hati za kusafiria za kidiplomasia na za kikazi pamoja na ushirikiano katika sekta ya afya.

Makubaliano hayo yalitiwa saini na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Balozi Téte António, wakati wa Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Angola uliomalizika jana Zanzibar.

Waziri January alisaini hati mbili za makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi na kuondoleana visa kwa wenye hati za kusafiria za kidiplomasia na za kikazi. Waziri Ummy alitia saini hati ya ushirikiano katika sekta ya afya.

Baada ya kutia saini hati hizo, Waziri January alisema Tanzania na Angola zina uhusiano wa kihistoria ulioanzishwa na viongozi wakuu wa kitaifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Agostinho Neto walianzisha uhusiano huo kwa matarajio ya kutoa manufaa kwa nchi zote mbili.

Katika mkutano huo, viongozi hao walijadili masuala mbalimbali ya uhusiano wa kisiasa, ulinzi, elimu, afya, mafuta na gesi, uchumi wa buluu, usafiri wa anga, kubadilishana visa, kusafiri bila visa kati ya nchi hizo mbili na hatimaye kuingia makubaliano ya ushirikiano.

Viongozi hao pia wamekubaliana kuyafanyia kazi masuala mbalimbali hususan kuwapo ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi Luanda pamoja na kufanya kongamano la biashara na uwekezaji na kuziwezesha sekta binafsi kufanya kazi kwa pamoja na ushirikiano zaidi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Balozi António, alisema Angola imefurahishwa na uamuzi wa Serikali ya Tanzania kukubali kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) na kuelezea utayari wake wa kushirikiana katika nyanja walizokubaliana kwa maslahi ya pande zote mbili.

"Tanzania na Angola ni marafiki wa siku nyingi, kupitia makubaliano tuliyotia saini leo (jana) tumefungua ukurasa mpya wa ushirikiano baina ya mataifa yetu.

"Tunaahidi kuyatekeleza yale yote tuliyokubaliana katika mkutano wetu ili kuendelea kuimarisha ushirikiano wetu," alisema Balozi António.

## MNH yamwokoa mtoto aliyemeza ushanga

**Na Gwamaka Alipipi**

JOPO la madaktari kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), limefanikiwa kuokoa maisha ya mtoto wa miaka mitano (jina limehifadhiwa) aliyekuwa amemeza ushanga wa plastiki na kukwama katika pafu kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Daktari Bingwa wa Mapafu na Mfumo wa Upumuaji kutoka MNH, Dk. Mwanaada Kilima, alisema walimpokea mtoto huyo hivi karibuni baada ya hali yake kuzidi kuwa mbaya.

Alisema walimfanyia vipimo vya uchunguzi ikiwamo kumpiga picha ya kamera na kubaini kipande cha ushanga katika moja ya mapafu ya mtoto huyo.

"Ni matukio yanayotokea mara kwa mara hata kwa watu wazima, utakuta mtoto anakohoa kila wakati, akipewa dawa kikohozi hakiponi kumbe amemeza kitu ambacho kinamletea madhara katika mfumo wake wa hewa," alisema Dk. Mwanaada.

"Hata mwezi uliopita tulimpokea mtoto wa miaka 11 kutoka Arusha ambaye alikuwa amemeza kipande cha plastiki cha bastola na aliishi nacho kwa miaka miwili katika mapafu, sasa wazazi wamehangaika sana kumtibu kikohozi."

Dk. Mwanaada alisema walipompokea mtoto huyo wiki iliyopita jopo la madaktari lilikutana na kuanza kumfanyia uchunguzi na kubaini kipande hicho cha ushanga katika pafu lake la kulia.

Aidha, alisema ushanga huo uliingia kwenye pafu alipokuwa akiuchezea mdomoni takribani mwezi mmoja uliopita bila wazazi wake kufahamu.

Alisema mtoto huyo alitaabika tangu wakati huo kwa kikohozi na kupumua kwa shida, huku njia mbalimbali zikitumika kujaribu kuitoa na kugonga mwamba, ndipo wataalamu wa mapafu walipofanikiwa kuitoa bila madhara yoyote.

"Tulitumia mpira laini wenye kamera ya video ya mapafu na kifaa cha kukamatia na kufanikiwa kuitoa hivyo kumwepusha na upasuaji mkubwa ambao ungesababisha ama kutoa pafu au sehemu ya pafu," alisema Dk. Mwanaada.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao na kuwachunguza kila wakati.

Pia, alisema mtu anaweza kumeza kitu katika mfumo wa hewa na akawa salama, lakini inategemea aina na kitu alichomeza.

"Kama mtu amemeza kitu kidogo ambacho kinaweza kupita katika tundu la hewa uwezekano wa kupona upo, lakini akimeza kitu kikubwa na kikaenda kuziba mfumo wa hewa anaweza kufariki," alisema Dk. Mwanaada.

Alisema upasuaji wa mtoto huo ulishirikisha timu ya wataalamu akiwamo Dk. Ramadhan Hamis, ambaye ni bingwa wa upasuaji wa kifua na moyo pamoja na Dk. Charles Komba ambaye ni bingwa wa upasuaji kifua pamoja na yeye.

HABARI KITAIFA

# Shule ya sekondari 'yamchokoza' waziri

**Na Waandishi Wetu**

IKITIMU wiki moja tangu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda apige marufuku shule kuweka michango ya lazima inayowanyima watoto fursa ya kwenda shuleni, kinyume chake shule zinatoza, Nipashe imebaini.

Katika kauli yake Januari 9, mwaka huu jijini Dodoma, Waziri Mkenda alitamka "Ni marufuku kwa shule yoyote kuweka michango ya lazima ambapo mzazi au mtoto asipotoa mchango huo, mtoto atakatazwa kwenda shuleni..."

Hata hivyo, uchunguzi wa Nipashe umebaini kwamba katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga ambayo ni ya bweni, mwanafunzi anayeripoti anatakiwa kulipa Sh. 65,000 ikitajwa kuwa ni 'mchango wa uendeshaji shule'.

Vilevile, katika nakala ya fomu hiyo ambayo Nipashe imeiona, inajumuisha malipo mengine ya tahadhari (Sh. 5,000); nembo (Sh. 5,000) na kitambulisho cha shule (Sh. 5,000) hivyo kufanya jumla ya michango ya lazima shuleni kuwa Sh. 80,000 kwa kila mwanafunzi.

Likirejewa agizo lake Waziri Mkenda, alielekeza "mtoto asirudishwe nyumbani kwa kutochangia dawati au chochote".

Aliendelea "Rais wetu, Samia Suluhu Hassan amekamilisha utaratibu wa kutoa elimu bila ada mpaka kidato cha sita. Hatutarajii mzazi aambiwe atoe mchango wa lazima."

Katika kinachoendelea kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga, mwandishi wa habari hizi alipowasiliana na Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, alimrejea Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga alitolee ufafanuzi Mkuu huyo wa shule, Mwalimu Nurah Kamuntu, alitolea uamuzi huo, akisema ni kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iliyoelekeza mchango huo wa Sh. 65,000.

"Kiasi hiki cha fedha, Sh. 65.000 kimepitishwa na TAMISEMI kwa shule zote za bweni, hata ukiangalia kwenye website (tovuti) ya TAMISEMI utaikuta fomu hiyo ya kujiunga na kiasi hicho cha fedha Sh. 65,000 kwa ajili ya maendeleo ya shule," alisema Nurah Kamuntu.

Alipotafutwa na Nipashe jana jioni kwa simu kuzungumzia suala hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alisema "hakuna mchango wowote, na mtoto yeyote haruhusiwi kupokewa kwa kumwekea masharti. Anatakiwa aende shuleni na aanze masomo mara moja. "Na wao wenyewe (shule) watafute fedha, na tumewaelekeza wakuu wa mikoa watafute fedha kuhakikisha watoto hawa wanapata chakula.

"Sisi serikali, Mheshimiwa Rais anatoa mabilioni kila mwezi. Ameshalipa gharama zote. Mtoto anayekwenda shuleni kokote nchini, apelekwe bila masharti yoyote. Kuhusu shule hii (Shinyanga Girls) ninaifuatilia sasa hivi (jana saa 11:52 jioni)."

Kuanzia Januari 2016, serikali ilipoanza kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada, maarufu Elimu Bure, ada ya shule ilifutwa kwa wanafunzi wa kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne, serikali ikigharamia takribani Sh. bilioni 23 kila mwezi.

Vilevile, Juni 2022, alipowasilisha makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23, Waziri wa Fedha na Mipango (wakati huo), Dk. Mwigulu Nchemba, alipendekeza kufutwa ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita ili kuwapunguzia gharama. Pendekezo hilo lilipitishwa na Bunge.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimsikiliza Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Katoliki Mbeya, Prof. Romuald Haule (kushoto), alipotembelea moja ya darasa la mihadhara, baada ya kukifungua chuo hicho, mkoani Mbeya jana. Katikati ni Mkuu wa Chuo hicho na Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga. **PICHA: OWM**

# Samia kuanza ziara mikoa minne Unguja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufanya ziara ya kichama katika mikoa minne ya Unguja itakayoanza leo.

Akizungumza na waandishi wa habari Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, alisema ziara hiyo itaanza Mkoa wa Kaskazini Unguja na kuwataka wananchi kujitokeza ili kueleza changamoto zao na kupatiwa ufumbuzi.

Alisema Rais Samia atashiriki shughuli mbalimbali na kukagua miradi ya maendeleo ya kichama.

Akizungumzia kuhusu vikao vya wajumbe wa Halmashauri Kuu vilivyofanyika visiwani humo kwa siku nne, alisema jambo jema bora na muhimu ambalo halijawahi kutokea katika chama, wajumbe kukutana na kuwasikiliza mawaziri wa sekta husika kuelezea miradi ya maendeleo wanayotekeleza.

Pia alisema wajumbe walipata nafasi ya kusikiliza na kujadiliana mipango inayofanywa na mashirika ya umma ikiwamo daraja la Magufuli, utekelezaji wa ilani kwa Zanzibar.

Alisema semina hiyo iliongeza uwelewa wa wajumbe wa Halmashauri Kuu na semina hiyo iliridhiwa na mwenyekiti ili kutoa nafasi ya uwelewa wa ushiriki.

Akizungumzia sherehe za miaka 47 kuzaliwa kwa CCM alisema, zitafanyika katika wadi nchi nzima kuhakikisha wanachama wanashiriki kikamilifu na kuoneshwa miradi yote inayotekelezwa.

"Wajumbe wa Halmashauri Kuu wamempongeza Dk. Samia kwa anavyojenga maridhiano na kufanikisha ushirikishaji wa taifa moja bila ya kubagua na kazi nzuri inayofanywa na Dk. Mwinyi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisema.

Makonda alisema, CCM ndio chama pekee barani Afrika chenye uwezo wa kubadilika kulingana na mahitaji yaliyopo.

Alisema ni chama kinachokubali kujikosoa na kukosolewa na hilo liliundwa na viongozi waasisi wa chama hicho akiwamo Mwalimu Nyerere na Mzee Karume waliliona hilo ili kupiga hatua.

Alisema jambo muhimu kwa chama kutambulika kwa uhitaji wa mtu na kiongozi ambaye anadumu kwa muda mrefu ni yule anayeweza kutambulika.

"Ikifika wakati wanataka watu wapole au wakali katika chama wanapatikana na nchi ikihataji mtu mkali au mpole tunawapatia, CCM ina kila mtu anayehitajika," alisema.

Alisema chama hicho ndicho chenye hazina ya watu wenye sifa zote na viongozi wenye uhitaji.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.01.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya **Ijumaa tarehe 19-01-2024 hadi tarehe 22-01-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 687 DUB /T 390 DHQ, T 453 DYG /T 887 DJB, T 853 DXS T 837 DJB, T 631 DFA /T 269 DUH, T 496 ECF /T 273 DUH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 4.70**
   **Kimo - mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: ***Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero*** kupitia Mikumi, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.01.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 18-01-2024 hadi 20-01-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga kupitia Mlandizi** gari hiyo ina namba za usajili: **T 458 DYG /T 387 DHQ**

2. Gari hizo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 5.10**
   **Kimo - mita 4.80**

3. Njia zitakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga** kupitia Mlandizi gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

HABARI KITAIFA

# Mawaziri Tanzania, Kenya waingilia kati zuio la ndege

**Na Restuta James**

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje wa Tanzania na Kenya, wameingilia kati mvutano wa Mamlaka za Anga za nchi hizo ambazo zimepiga marufuku ndege za kila upande kutua kwenye viwanja vyake vya Nairobi na Dar es Salaam.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba na mwenzake wa Kenya, Musalia Mudavadi, waliandika katika akaunti zao za mtandao wa X kwamba wamewasiliana na tayari sintofahamu hiyo inashughulikiwa na mamlaka za anga.

"Nimezungumza na mwenzangu wa Kenya, Musalia Mudavadi na tumekubaliana kwamba vikwazo vya usafiri wa anga kati ya nchi zetu na kutoka nchi yetu yoyote hadi nchi ya tatu havipaswi kuwapo. Kupitia mamlaka zetu, tumeamua kumaliza suala hili ndani ya siku tatu," aliandika Makamba.

Waziri Mudavadi, aliandika "Jioni ya leo (juzi), nimezungumza na Makamba kuhusiana na uamuzi wa TCAA kufuta vibali vya KQ kuendesha safari za abiria kati ya Nairobi na Dar. Tumekubaliana kwa pamoja kwamba Mamlaka zetu za Usafiri wa Anga zitashirikiana ili suala hilo litatuliwe kwa amani ndani ya siku tatu zijazo."

Hayo yametokea siku moja baada ya TCAA, kuzuia ndege za KQ kutua kwenye viwanja vya ndege vya Tanzania kuanzia Januari 22, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, alitoa zuio hilo juzi ikiwa ni njia ya kujibu uamuzi wa Mamlaka ya Anga ya Jamhuri ya Kenya kuzuia ndege za mizigo ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kutua Kenya.

Katika tamko hilo, Johari alisema hatua ya Kenya kuzuia ndege ya ATCL imevunja Ibara ya 4 ya mkataba wa makubaliano ambayo nchi hizo ziliingia mwaka 2016.

"Serikali ya Tanzania siku zote inaheshimu makubaliano ya Chicago ya mwaka 1994 kuhusu makubaliano ya usafiri wa anga baina ya nchi mbili," alisema Johari katika taarifa yake juzi.

Hata hivyo, baadaye jana jioni, Johari alitoa taarifa umma, akiuarifu kwamba mamlaka ya Kenya imetoa rukhsa kwa ndege za mizigo za Tanzania kutua Kenya, hivyo TCAA imefuta kusudio lake la kuzuia ndege za abiria za Kenya kutua nchini.




Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Abeida Rashid Abdullah (katikati), akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Said Omar Shaaban, kwa mchango na mawazo yake ya kuendeleza Baraza la Udhibiti Mfumo wa Utoaji wa Leseni, katika hafla iliyofanyika Nyamanzi mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB, UNDP kujengea uwezo wajasiriamali fursa za AfCFTA

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuimarisha uwezo wake na ushirikishaji wa wadau, Taasisi ya CRDB Bank Foundation imetia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Mkataba huo wa miaka mitano unakusudia kufanikisha uwezeshaji wananchi hasa wajasiriamali vijana na wanawake, upatikanaji rahisi wa mtaji wa kukuza na kuendeleza biashara, ukuzaji wa biashara changa za kibunifu pamoja na kubadilishana uzoefu.

Ushirikiano huu wa kimkakati kati ya Taasisi ya CRDB Bank Foundation na UNDP unadhihirisha juhudi za pamoja zinazolenga kukabiliana na changamoto zilizopo ili kuwezesha ukuaji jumuishi wa uchumi na utekelezaji wa Malengo Endelevu nchini.

Makubalino hayo yanafungua milango ya utekelezaji wa miradi ya kuwezesha usawa wa kijinsia katika fursa za uchumi na biashara, kuwajengea vijana uwezo, ujumuishaji wananchi katika huduma za fedha na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ikiwa na zaidi ya biashara changa, ndogo na za kati milioni tatu zinazochangia asilimia 27 kwenye Pato la Taifa huku nyingi zikimilikiwa na wanawake, Tanzania ina nafasi nzuri ya kunufaika zaidi na ushirikiano wa kimkakati kama huo ulioingiwa kati ya Taasisi ya CRDB Bank Foundation na UNDP kwa kuwawezesha wananchi hasa vijana na wanawake wajasiriamali kunufaika na fursa zilizopo katika Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA).

Akizungumza katika hafla ya kutia saini makubaliano hayo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Ether Mwambapa alisema biashara changa, ndogo na za kati zina mchango mkubwa kwenye uchumi wa taifa na kipato cha mwananchi mmojammoja, hivyo kuhitaji mkakati makini wa kuzilea na kuzikuza.

"Uchumi wa taifa letu unazitegemea biashara changa, ndogo na za kati kwa kiasi kikubwa. Sekta hii inaajiri zaidi ya watu milioni tano, hawa ni vijana na wanawake ambao hawawezi kuzifikia fursa za kiuchumi zilizopo sokoni.

"Kwa kulitambua hili, Taasisi ya CRDB Bank Foundation ilibuni na kuitambulisha Programu ya Imbeju inayowaelimisha vijana na wanawake namna ya kuendesha biashara kisasa na kutoa mtaji wezeshi. "Kushirikiana na UNDP kunadhihirisha utayari wetu wa kuyabadili na kuyaboresha maisha ya mjasiriamali wa Tanzania tukianza mwaka mpya, 2024," alisema Tully.

Mkurugenzi huyo alisema tangu Programu ya Imbeju ilipozinduliwa mapema mwaka jana, tayari mafunzo yaliyotolewa yamewanufaisha zaidi ya wanawake 100,000 huku mtaji wezeshi wa zaidi ya Sh. bilioni tano ukiwa umetolewa kwa wajasiriamali waliokidhi vigezo.

Alisema mkataba huo wa makubaliano pia unaendana na malengo ya Taasisi ya CRDB Bank Foundation katika kutekeleza Malengo Endelevu ya Dunia (SDG) hasa lengo namba moja linalolenga kuondoa umaskini, lengo namba tano linalohamasisha usawa wa kijinsia pamoja na ajira kwa wote kama ilivyoainishwa kwenye lengo namba nane.

Mwakilishi Mkazi wa UNDP nchini, Shigeki Komatsubara alisema kuwa wakati wote, shirika hilo linajielekeza kufanikisha utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Dunia.

"UNDP inafanya kila iwezalo kuwezesha utekelezaji malengo endelevu kwa kuweka mazingira rafiki ya kuimarisha kipato, kuwa na jamii inayojitegemea na kuhamasisha utawala bora.

"Mambo haya ndio yanayojenga msingi wa matendo yetu, hivyo ushirikiano huu tunaousaini leo (jana) unaonesha utayari wetu wa kufungua fursa kwa wananchi," alisema Komatsubara.

Katika kuyafikia malengo, Komatsubara alisema ni muhimu kuwa na ushirikiano wa wadau wenye maono sawa.

"Tukianza safari hii ya ushirikiano, ni furaha kuona kuwa tunaelekea kwenye kutimiza ndoto ya kuacha alama kwa kuchangia mabadiliko chanya kwa jamii.

"Ushirikiano unaozihusisha taasisi kubwa ni muhimu ili kujenga misingi ya kesho iliyo sawa kwa wote, endelevu na yenye uchumi shirikishi," alisema Komatsubara.

Ushirikiano wa Taasisi ya CRDB Bank Foundation na UNDP ambazo zote zinazo programu zinazowalenga vijana na wanawake, unatarajiwa kufungua fursa nyingi zaidi kwa wajasiriamali wadogo wa Tanzania, hasa vijana na wanawake, kunufaika na soko pana lililomo ndani ya AfCFTA.

Wakati Taasisiya CRDB Bank Foundation ikiwa na Imbeju, UNDP inao mradi wa Funguo unaowajengea uwezo vijana wabunifu.

## Wazindua mfumo wa kidijitali kutoa motisha watoa huduma

**Na Halfani Chusi**

KAMPUNI ya Pesapal imezindua mfumo mpya katika huduma yake ya vifaa vya malipo ya mtandaoni (POS), sasa mteja atatoa malipo ya shukrani kwa mtu aliyempa huduma.

Mfumo huo tayari upo kwenya vifaa vyake vya Pesapal Sabi POS ikilenga kurahisisha malipo ya shukrani (tip) huku ikiendelea kuondokana na malipo ya fedha taslimu kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki.

Meneja Mkazi wa Pesapal Tanzania Limited, Bupe Mwakalundwa, alielezea umuhimu wa utamaduni wa utoaji malipo ya shukrani kwenye sekta ya huduma na mashine za Sabi POS utakavyochangia uwazi na ufanisi katika sekta hiyo.

"Tumejizatiti kukuza utamaduni unaotambua na kukubali huduma zinazotolewa na wafanyakazi wa kampuni mbalimbali. Hatua hii si tu kwamba itaongeza motisha kwao, bali pia ni muhimu katika kuchangia kuwafanya waridhike na kazi zao," alisema.

Alisema kwa kutumia machine hizo, wateja wamepewa uwezo wa kuonesha ukarimu na kukubali huduma za kipekee.

Mwakalundwa pia alisisitiza ni utamaduni kwa nchi zilizoendelea - mfanyakazi wa kampuni ya utoaji huduma kupata kipato cha ziada kupitia malipo ya shukrani, hali inayochangia kuboresha maisha yao. Pesapal inajizatiti kufanya hivyo Tanzania.

"Tumejizatiti kukuza utamaduni unaotambua na kuthamini huduma bora zinazotolewa na wafanyakazi katika kampuni mbalimbali. Mbinu hii si tu inainua ari yao, bali pia inachangia kwa kiasi kikubwa kuridhika kwao na kazi zao kwa ujumla," alisema.

Meneja huyo alisema mashine yao ya Sabi POS inasimama kama uthibitisho wa dhamira hiyo, ikitoa njia rahisi kwa wateja kutambua na kutunuku huduma ya kupigiwa mfano na kuimarisha maadili ndani ya tasnia ya huduma nchini.

"Tunatoa njia rahisi kwa wateja kuonesha kuthamini kwao huduma bora," Mkurugenzi wa Kiufundi wa Pesapal, Fred Mwangima, alisema.

Kwa mujibu wa McKinsey Global Payment Map, soko la ndani la malipo ya kielektroniki barani Afrika linatarajiwa kuona mapato yakikua kwa takriban asilimia 20 kwa mwaka, na kufikia karibu Dola bilioni 40 ifikapo mwaka 2025.

"Tunashughulikia mienendo ya sasa ya hali ya malipo ambayo imeona kuongezeka kwa malipo ya kidijitali. Kutoa ushauri ni kichocheo kikubwa kwa wahudumu kutoa huduma bora, lakini imekuwa vigumu zaidi katika enzi ya baada ya UVIKO-19 kwani watumiaji wengi wanahamia kwenye shughuli zisizo na fedha taslimu," Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Pesapal Group, Agosta Liko, alisema.

Katika miaka ya karibuni, wafanyabiashara katika tasnia nyingi, ikijumuisha huduma za ukarimu, burudani, huduma za afya na vituo vya mafuta, wamekumbatia teknolojia ya kidijitali. Maendeleo katika kukubali malipo yakidijitali yamesababisha matokeo chanya. Tunaimani malipo ya kidijitali yataongezeka na kupata msukumo zaidi kupitia mfumo huu mpya tuliyozindua.

Wauzaji ambao tayari wana mashine zao, wanaweza kupata mfumo huu kwa urahisi kupitia njia rahisi ya programu ya mtandao.

HABARI KITAIFA

# Katibu Mtendaji MCT aanika mikakati yake

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mtendaji mpya wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura, ameanza kazi rasmi huku akiweka wazi mikakati yake minne ukiwamo wa kulinda na kusimamia uhuru wa vyombo vya habari.

Sungura aliweka wazi mikakati yake jana wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, ikiwa ni siku yake ya kwanza katika ofisi hiyo iliyoko Tegeta, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Baada ya kuripoti, sungura alipokewa na mtangulizi wake, Kajubi Mukajanga, aliyehudumu kwa miaka 15 katika nafasi hiyo, ambaye Septemba 28, mwaka jana alitangaza kuachia wadhifa huo ndani ya miezi mitatu baadaye.

Sungura alitambulishwa kwa wafanyakazi 12 wa MCT kati yao, 10 wakiwa Dar es Salaam na wawili wa Zanzibar.

Katibu Mtendaji huyo mpya alianika mkakati wake mwingine ni kusimamia weledi, maadili kwa vyombo vya habari na wanahabari kwa kuhakikisha viwango vinapanda zaidi.

"Ili kufanikisha hilo, tutafanya utafiti kwa kuzungumza na wadau na kujua maeneo gani ya kupandisha viwango hivyo," alibainisha.

Mkakati mwingine, aliutaja kuwa ni nguvu ya kiuchumi huku akibainisha kuwa vyombo vingi vya habari vinatetereka kwa sababu ya tatizo hilo, hivyo kwa kushirikiana na wenzake, wataangalia ni kwa namna gani watasaidia kulikwamua tatizo hilo.

"MCT tutaendelea na usuluhishi, badala ya vyombo vya habari kupelekwa mahakamani, tutaendelea kufanya usuluhushi," alisema.

**SUNGURA NI NANI?**

Kwa mujibu wa Mtandao wa Uandishi wa Habari za Uchunguzi wa Global (GIJC), Sungura, Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), ni mwanahabari mahiri kutoka Tanzania na mtaalamu wa masuala ya habari akiwa na uzoefu wa miaka 22 ndani na nje ya nchi.

Miongoni mwa maeneo ambayo amebobea kwenye taaluma hiyo ni pamoja na uandishi wa habari za uchunguzi, usimamizi wa programu na ruzuku pamoja na ukuzaji wa biashara ya vyombo vya habari kwa uchapishaji na utangazaji.



Ni miongoni mwa wanaoamini kwa dhati kuwa 'fedha hutoka kwenye chumba cha habari' na kwamba ili sekta ya habari ijitegemee na kupata heshima, ni lazima iwekeze katika kujenga kuthaminiwa na kuaminiwa kwa umma kupitia uandishi bora wa habari.

Kabla ya kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TMF, Ernest aliwahi kuwa Meneja na Mkurugenzi Mtendaji wa mradi wa Hivos Tanzania Media Fund.

Pia amewahi kuwa Mkuu, Mkurugenzi wa Fedha na Mkurugenzi wa Masomo katika Taasisi ya Elimu ya Vyombo vya Habari Tanzania (TIME) na Mhariri wa Habari na mwandishi wa uchunguzi wa Gazeti la The Guardian, Tanzania.

Alikuwa mwanahabari wa kwanza nchini Tanzania kuwa na Shahada ya Kwanza na Uzamili katika Utawala wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

# Bil. 48/- kusomesha wanafunzi stashahada

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema katika mwaka wa masomo 2023/24 serikali imetenga Sh. bilioni 48 kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada.

Amesema mpango huo ambao ni maono na maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, unalenga kuhakikisha elimu inayotolewa inakuwa bora na kuwezesha wahitimu wa vyuo nchini kujiamini na kumudu ushindani wa kitaifa na kimataifa.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa Chuo Kikuu Katoliki Mbeya (CUoM) mkoani Mbeya huku akibainisha kuwa lengo lingine la Rais Samia ni kuona vijana wengi wanapata elimu itakayowapa ujuzi na uwezo wa kushiriki katika ujenzi wa taifa.

Waziri Mkuu alisema serikali imetenga Dola za Kimarekani milioni moja kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ambazo zinasomesha wahadhiri 27 kutoka vyuo vikuu visivyo vya serikali.

Aliongeza kuwa fedha hizo pia zitatumika kugharamia wahadhiri saba katika ngazi ya Shahada ya Umahiri na 20 katika shahada ya uzamivu kwa programu za afya na sayansi shirikishi.

"Kupitia mradi huu, serikali imekuwa ikivifikia vyuo vikuu binafsi. Kitendo hicho kinaonyesha dhamira ya dhati ya serikali ya kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika utoaji wa elimu kwa ngazi zote. Hii ni kutokana na ukweli kwamba serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi katika utoaji wa elimu kuanzia ngazi ya awali hadi elimu ya juu," alisema.

Majaliwa alitoa wito kwa vyuo vinavyomilikiwa na taasisi zisizo za serikali kuweka mpango mkakati wa kuongeza idadi ya wanataaluma hususan maprofesa, wahadhiri waandamizi na wahadhiri kwa maeneo ya programu zinazotolewa.

Aidha, Majaliwa alisema serikali inathamini na kutambua mchango wa madhehebu ya dini likiwamo Kanisa Katoliki kwa kuwa mstari wa mbele katika utoaji wa huduma kwenye sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, elimu na ustawi wa jamii.

Mwenyekiti wa Bodi la Baraza la Chuo hicho, Askofu John Ndimbo, aliishukuru Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa kuona umuhimu wa kukipa chuo hicho hadhi ya chuo kikuu baada ya kutimiza masharti yote.

"Kupitia tume maalum iliyoundwa na TCU ilijiridhisha na uboreshaji wa miundombinu ndipo tulipewa hadhi ya chuo kikuu, TCU imekuwa mlezi bora kwetu," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula, ambaye alimwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kwenye ufunguzi huo, alilipongeza Kanisa Katoliki linavyowekeza kwenye sekta ya elimu.

# Jela miaka mitatu kwa kuharibu vifaa kanisani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imemhukumu Elpidius Edward (26) kifungo cha miaka mitatu jela kwa kosa la kuharibu vitu mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 48, mali ya Kanisa Kuu Jimbo Katoliki la Geita.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama, Johari Kijuwile baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Kijuwile alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kuharibu vitu vya kanisa kama yake.

Hakimu Kijuwile alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Scolastica Teffe ulipeleka mahakamani mashahidi sita na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo.

"Mshtakiwa mahakama hii imekutia hatiani kwa kosa la kuharibu mali za kanisa. Pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili kukupunguzia adhabu," alisema Hakimu Kijuwile kabla ya kutoa hukumu. .

Mshtakiwa alijitetea kuwa anaomba mahakama impunguzie adhabu kwa sababu ni kosa lake la kwanza.

Hata hivyo, Wakili Teffe aliomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Baada ya ombi hilo, Hakimu Kijuwile alisema mshtakiwa atakwenda jela miaka mitatu ili akajifunze tabia ya kuishi na jamii na ana imani kwamba akimaliza kifungo atakuwa raia mwema kwa jamii.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili Scolastica Teffe alidai kuwa Febuari 26, mwaka jana, katika mtaa wa Mbugani mkoani Geita, mshtakiwa alivunja Kanisa Kuu Jimbo Katoliki la Geita na kuingia ndani kisha kuharibu vitu mbalimbali vyenye thamani zaidi ya Sh milioni 48 mali ya kanisa hilo, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.01.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 18-01-2024 hadi 20-01-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga kuelekea Dar es Salaam** kupitia **Mlandizi** gari hizo zina namba za usajili: **T 778 EAP /T 568 EAZ, T 262 EDD /T 572 EAZ, T 327 EDD /T 416 AYQ, T 331 EDD /T 390 DHQ, T 986 EDR /T 321 DDH, T 118 EAG /T 881 EAU**

2 Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22.00**
**Upana - mita 4.30**
**Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga kupitia Mlandizi** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.01.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 19-01-2024 hadi 22.01.2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar- Es- Salaam Port kuelekea Mzenga,** gari hizo zina namba za usajili: **T 112 EAG / T 777 AQR, T 792 DYL / T 394 DVS, T 249 EAZ /T 499 DZX**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22.00**
**Upana - mita 7.30**
**Kimo - mita 4.80**

2. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar-Es-Salaam** hadi **Mzenga** kupitia **Morogoro** Road Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka Dar- Es- Salaam Port mpaka Mlandizi Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga gari zitasafiri muda wa mchana ***(kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hadhari kubwa inatakiwa kuepuka kipindupindu Dar

**KILA** msimu wa mvua unapofika, mara kwa mara ugonjwa wa kipindupindu umekuwa ukiripotiwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dae es Salaam huku sababu kubwa ikitajwa kuwa ni uchafu. Mwaka jana kwa mfano, moja ya maeneo yaliyotajwa kuathirika na tatizo hilo ni Wilaya ya Ilala baada ya watu 10 kugundulika kuwa na ugonjwa huo.

Kutokana na uwapo wa tishio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameshatangaza operesheni ya kufanya usafi katika maeneo mbalimbali huku akibainisha kuwa taasisi mbalimbali zitashiriki katika mpango huo.

Tishio la kipindupindu Dar es Salaam linaibuka huku mikoa ya Mwanza na Shinyanga ikiwa imeshatikiswa baada ya kuwapo kwa vifo, wengine kubainika kuwa na ugonjwa na mamia kuwekwa katika karantini. Katika mkoa wa Mwanza iliripotiwa wiki iliyopita kuwa watu 34 walithibitika kuwa na kipindupindu huku Shinyanga ikielezwa kuwa watu watano walifariki dunia na wengine 452 kuwekwa katika karantini.

Taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kutokana na ugonjwa huo ni kwamba sababu kubwa ni uchafu unaotiririka katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye mfereji wa Kirumba.

Wahenga wanasema ukiona mwenzako ananyolewa tia kicha chako maji. Msemo huo unasadifu na hali ya sasa kuhusu kuwapo kwa kipindupindu katika maeneo mbalimbali ya nchi kutokana na mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha kuwapo uchafu kwenye baadhi ya maeneo, ambao ndio chanzo halisi cha maradhi hayo.

Kama mikoa mingine ilivyoguswa, Dar es Salaam nayo iko katika hatari kutokana na hali halisi ya miundombinu na mpangilio wa makazi katika sehemu tofauti. Baadhi ya wananchi wa mkoa huo, hutumia fursa ya mvua kufungulia vyoo na kutiririsha maji ovyo kwenye mitaro na barabarani. Hapo ndipo tatizo huanzia kwa watu kwenye baadhi ya maeneo kuugua kipindupindu.

Alivyotangaza RC Chalamila kuhusu usafi, hiyo ndiyo njia pekee itakaowanusuru wakazi wake dhidi ya kipindupindu. Kila mwananchi katika eneo lake anapaswa kufanya usafi bila kushurutishwa na mamlaka yoyote ya serikali. Kwa maneno mengine, hakuna mbadala wa usafi katika kupambana na kipindupindu.


Kutokana na mvua iliyonyesha hivi karibuni, baadhi ya maeneo katika mkoa wa Dar es Salaam miundombinu imeharibika vibaya na katika baadhi ya makazi ya watu maji hayakauki hata kama mvua itapungua. Hiyo ni kutokana na watu kufungulia vyoo na kutiririsha maji machafu yanayopita kwenye makazi ya watu na kwenye barabara.

Pamoja na kuwapo kwa hali hiyo, viongozi wa serikali za mitaa katika maeneo hayo wanafumbia macho vitendo hivyo hali inayohatarisha afya za watu. Ni wazi kwamba kama hali itaendelea hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa maeneo kadhaa kukumbwa na mlipuko wa kipindupindu.

Ni wajibu wa viongozi wa serikali za mitaa hasa kamati za mazingira, kupita na kukagua nyumba zinazoendekeza mtindo wa kutiririsha maji machafu kila mvua inaponyesha na wale watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria kuhusiana na uchafuzi wa mazingira.

Ni vyema kila mwananchi ndani ya mkoa wa Dar es Salaam akachukua hatua za kuweka mazingira katika hali ya usafi ili kuepuka maradhi ya kipindupindu. Kama kila mmoja atatimiza wajibu wake, ni dhahiri kwamba Dar es Salaam bila kipindupindu inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Meza ya mazungumzo iepushe maandamano ya CHADEMA

**CHAMA** cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kinajiandaa kufanya maandamano kwa lengo la kushinikiza serikali izingatie maoni na mapendekezo ya wadau wa uchaguzi.

Maandamano hayo yanatarajiwa kufanyika Januari 24, huku Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ikiwa katika hatua za kukamilisha miswada ya sheria iliyosomwa bungeni mwishoni mwa mwaka jana.

Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Muswada wa mwaka 2023 na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, anasema chama hicho hakijaridhishwa na miswada hiyo iondolewe bungeni kwa kuwa haikuzingatia maridhiano.

Mbowe anasema, kwa muda mrefu amepigania maridhiano na CCM, huku akipingwa na viongozi wenzake wa CHADEMA, na kwamba hakutarajia kuwapo kwa miswada hiyo bungeni.

Wakati CHADEMA inatangaza kuandamana Januari 24, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila anasema kuanzia Januari 23 hadi 24 zitakuwa ni siku za kufanya usafi.

Kauli hiyo inaonyesha kuwa kunaweza kuwapo sintofahamu kati ya serikali ya mkoa na hao walioandaa maandamano, hivyo ninadhani busara ingetumika kumaliza mkwamo uliopo.

Njia hiyo ni serikali na CHADEMA kukaa meza moja ya mazungumzo na kujadili kwa kina mkwamo wa kisiasa kuhusu miswada hiyo ya sheria ambayo tayari imefikishwa bungeni.

Hivyo, CHADEMA ingesitisha kwanza maandamano na kutafuta njia hiyo ya kukutana na serikali kuelezea mtazamo wao kuhusu miswada hiyo ili hatimaye pande mbili zikifikie muafaka.

Kwa kawaida, mazungumzo ya pamoja huwa ni njia nzuri ya kukwamua jambo ambalo limekwama, hasa kama pande mbili zinazotofautiana zinaposhirikisha watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini.

Ingawa ni haki kuandamana, lakini CHADEMA wangeacha kwanza maandamano na kutafuta suluhu kwa njia ya kukaa pamoja, ili kila upande uelezee kero zake ili hatimaye kufikia muafaka.

Lakini ikumbukwe kuwa pamoja na kwamba ni maandamano ya amani, wakati mwingine yanaweza kuingiliwa na wasiokitakia mema chama hicho na kusababisha uharibifu wa mali za watu.

Hivyo, hata kama chama hicho kimefanya mazungumzo mengi ya maridhiano, ingekuwa ni vyema kisichoke, kiendelee na harakati hizo za kutafuta maridhiano kwa njia ya mazungumzo.

Hata kama kuna kutoridhishwa na mchakato wa ukusanyaji wa maoni juu ya miswaada hiyo, ninadhani viongozi wangendelea kutafuta nafasi ya kukutana na viongozi wa serikali.

Uamuzi wa kutangaza kufanya maandamano ya amani ya nchi nzima, kwa ajili ya kuishinikiza serikali kuondoa miswaada hiyo bungeni, unaweza kuwa sawa, lakini ni kuangalia athari zake.

Niligusia kidogo kwamba maandamano yanaweza kuwa ya amani, lakini yakaingiliwa na watu wengine wenye nia ya kupora mali za watu au kuharibu mali za watu, watakaolaumiwa ni CHADEMA.

Vilevile, wanaweza kulazimisha kuandamana na kukutana na nguvu za dola na kusababisha baadhi ya watu kuumia, ndio maana ninakazania umuhimu wa kukaa meza moja ili kufikia muafaka.

Meza ya mazungumzo inaweza kuepusha hayo yote na kufikia kile ambacho chama hicho kinakihitaji bila mtu kuumia wala watu kuharibiwa au kuibiwa mali zao mitaani.

Uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi maandamano ya amani huwa yanageuka kwa kuharibu na kupora mali za watu, kutokana na kwamba huingiliwa na watu wasio na nia njema.

## LATRA: Mizigo yote katika basi iandikwe jina la abiria

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imeagiza wenye mabasi kuhakikisha mizigo yote ya abiria inaandikwa majina ya abiria husika vinginevyo watatozwa faini.

Jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Usafiri wa Barabara wa mamlaka hiyo, Johansen Kahatano, aliagiza hayo alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusu viwango vya alama zitakazotumika kwenye mizigo ya abiria.

Alisema utaratibu huo unalenga kupunguza upotevu wa mizigo ya abiria na kuzuia usafirishaji mizigo haramu unakofanywa na baadhi ya watu kwenye mabasi.

Alisema LATRA imekuwa inafanya ukaguzi na itaendelea kufanya mara kwa mara na wale watakaokutwa hawajazingatia utaratibu, watatozwa faini ya Sh. 100,000.

Kahatano alisema awali kila mwenye basi alikuwa anaweka alama kwa mtindo wake; wengine wakiandika majina kwa kalamu, lakini LATRA imeandaa viwango ambavyo vitatumika kwa wenye mabasi wote.

"Ili kufuatilia utekelezaji wa agizo hili kwa urahisi tumeaandaa viwango vya kuweka alama kwenye mizigo ya abiria ambayo kila mtoahuduma ataifuata na lazima iwe na jina la abiria, anashukia wapi na tarehe ya kusafiri.

"Hiyo alama inakuwa na sehemu mbili, sehemu ya kwanza inabandikwa kwenye mzigo na nyingine anapewa abiria ili akishuka anaonesha tag yake anapewa mzigo wake tofauti na utaratibu wa sasa ambapo mtu anaonesha mzigo kwa kidole," alisema.

Alisema sheria hiyo ilipitishwa mwaka 2020, lakini utekelezaji wake ulianza mwaka jana japo kulitokea changamoto ya kila mtoahuduma kuweka tag hizo kwa viwango anavyojua mwenyewe.

Alisema LATRA iliamua kuja na utaratibu huo baada ya kuwa inapata malalamiko ya kupotea mizigo mara kwa mara kwenye mabasi na wakati mwingine abiria kuondoka na mizigo ambayo si yao.

"Wako watu wanapakia dawa za kulevya, mirungi, vipodozi na wanaoumia ni hawa wenye mabasi kwa sababu ikikamatwa mwenye mzigo hawezi kukubali kwamba ni wake, lakini kwa utaratibu huu mpya wa alama, mhusika hatakuwa na namna ya kuukana mzigo wake," alisema Kahatano.

LATRA ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na, 3 ya Mwaka 2019. Ni sheria iliyofuta sheria ya iliyokuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA).

# DC aunda timu kufuatilia wanaoozesha wanafunzi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, ameunda timu kufuatilia kwa karibu mienendo ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Parakuyo ili kudhibiti tabia ya baadhi ya wazazi wanaotorosha watoto na kuwaozesha.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya kiongozi huyo kufanya ziara ya kushtukiza shuleni huko. Shule hiyo inachukua wanafunzi wa jamii ya wafugaji wa kimasai.

Shaka alifika shuleni kuona idadi ya wanafunzi waliopokewa tangu Januari 8, mwaka huu, shule zilipofunguliwa.

Alisema shule hiyo imepangiwa wanafunzi wa kidato cha kwanza 59. Kati yao, wasichana ni 29, lakini walioripoti hadi siku ya pili baada ya shule kufunguliwa, walikuwa ni watano tu (wote wa kiume).

Shaka alisema kuwa wiki mbili kabla ya shule kufunguliwa kuanza mwaka mpya wa masomo, alipokea kesi mbili katika kata hiyo za wazazi ambao wamepokea ng'ombe ili kuwaozesha mabinti zao kabla ya matokeo kutangazwa.

Mkuu wa Wilaya alisema kesi nyingine ilihusu mtoto wa kike ambaye wazazi wake wametorosha kwa ujanja, wakidai ni mgonjwa, lakini ufuatiliaji ukabaini alipelekwa kwa mganga wa kienyeji.

"Binti siyo kwamba anaumwa, bali alipelekwa kwa mganga kimkakati kwa maana ya wazazi wanavuta muda ili baadaye waweze kwenda kumfugisha ndoa," alisema Shaka.

Pia alisema baadhi ya wazazi wamewapeleka kimkakati watoto wao wa kike mjini Morogoro katika shule ambazo hazijasajiliwa ili baadaye wawarudishe na kuwaozesha.

"Kuanzia sasa serikali tutakuwa wakali sana, hatutasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa mzazi yeyote atakayebainika kwa namna moja ama nyingine anamhujumu mtoto wake katika suala la kupata elimu," alisema.

Shaka aliwaagiza viongozi wa kata pamoja na diwani kuwafuatilia, hasa wa kike, ili kujua waliko kwa kuwa kuna tabia zilizojengeka za baadhi ya wazazi kuwatorosha watoto wao wa kike waliofaulu darasa la saba na kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza.

"Lengo ni tujue wako wapi? Je, wapo ndani ya jamii ya Parakuyo au wamepelekwa maeneo mbalimbali? Kama ndivyo, tuchukue hatua dhidi ya wazazi wao," alisema.

Diwani wa Parakuyo, Ibrahimu Kalaita, alisema bado ni mapema kujua watoto wa kike waliochanguliwa kujiunga kidato cha kwanza shuleni huko kama wamechepushwa au la.

"Ninajua muda uliowekwa kisheria bado na wazazi wanaendelea kujindaa kuwaleta watoto shuleni, lakini sisi viongozi wa kata tutaendelea kutekeleza maelekezo ya Mkuu wa Wilaya," alisema Kalaita.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, ambayo mwaka jana ilifanyiwa mapitio, sasa inaelekeza elimu ya msingi na sekondari kidato cha kwanza hadi cha nne ni ya lazima.




Mshindi wa Shindano la Maokoto linaloendeshwa na Kampuni ya bia ya Serengeti (SBL), Gracewell Sewando (katikati), akipokea mfano wa hundi ya 500,000/- kutoka kwa Meneja wa Airport Bar, Vaina James (kushoto), katika hafla iliyofanyika wilayani Gairo, mkoani Morogoro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Korti Kuu yaagiza kesi waliofungwa miaka 10 gerezani isikilizwe upya

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala ya Wilaya Kanda ya Morogoro imeamuru mashtaka dhidi ya Said Kanji na mwenzake waliofungwa miaka 10 gerezani kwa kukutwa na vifaa vya kuvunjia nyumba, yaanze kusikilizwa upya kwa hakimu mwingine.

Hukumu hiyo ya mahakama imetolewa mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro, Hadija Kinyaka baada ya kusikiliza rufani iliyowasilishwa na Kanji, akipinga hatia na adhabu aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Kilombero.

Kanji alitiwa hatiani pamoja na mwenzake Nikolaus Uliza kwa kosa la kukutwa na vifaa vya kuvunjia nyumba, bisibisi, mapanga mawili, tochi, koleo na kofia ya kuziba uso ndani ya begi jeusi saa sita usiku.

Inadaiwa katika maelezo ya onyo polisi, washtakiwa walikubali kukutwa na vifaa hivyo, lakini walikana kufanya uhalifu.

Kanji alikata rufani akiwa na sababu tisa ikiwamo mahakama ilikosea kumtia hatiani kwa ushahidi wa upande wa mashtaka ambao haukuthibitika na ilikosea kumtia hatiani kwa kuzingatia maelezo ya onyo ambayo aliandika polisi, akisisitiza hakuwa huru alipokuwa kituoni.

Kanji anadai ushahidi wa upande wa mashtaka ulikuwa dhaifu, mahakama iliegemea upande wa mashtaka wakati wa usikilizaji wa shauri na hivyo ilikosea kumtia hatiani kwa kosa la kukutwa na vifaa vya kuvunjia nyumba wakati hakuna shahidi hata mmoja kati ya watatu aliyesema vitu hivyo ni mali yake.

Mrufani alijiwakilisha mwenyewe, mjibu rufani aliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Shabani Kabelwa.

Wakili Kabelwa alidai upande wa Jamhuri ulithibitisha mashtaka dhidi ya mrufani bila kuacha shaka. Kabelwa anadai Julai 15, 2022, saa sita usiku, askari waligonga mlango anakokuwa anaishi mrufani, mlango ulifunguliwa na walipofanya upekuzi walikuta vifaa hivyo vya kuvunjia nyumba ndani ya begi jeusi.

Mahakama baada ya kusikiliza rufani, Jaji Kinyaka alisema ushahidi kwenye ukurasa wa 12, 15 na 17 wa mwenendo wa kesi ni wazi kwamba unafanana, mshtakiwa alipopekuliwa alipatikana na zana za kuvunja nyumba.

Ilibainika zaidi kuwa mrufani na mshtakiwa wa pili walifukuzwa na shahidi wa kwanza na shahidi wa tatu saa tano usiku wakiwa doria.

Washtakiwa hao waliingia katika nyumba iliyopangishwa na mrufani, wote walikamatwa na kupekuliwa saa sita usiku na kupatikana na vyombo vya kuvunja nyumba.

"Kutokana na uchunguzi wa kile kilichotokea katika mahakama, ni salama kushikilia kwamba ikiwa watuhumiwa watashtakiwa chini ya kifungu cha 298 (c) cha Kanuni ya Adhabu, ushahidi wa mdomo wa mashahidi wa upande wa mashtaka, ulitosha kuanzisha kosa chini ya kifungu hicho .

"Kutokana na matokeo ya hapo juu, ni wazi kwangu kwamba upande wa mashtaka ulitakiwa kuwashtaki watuhumiwa kwa kumiliki vyombo hivyo ili wathibitishe kama wanamiliki kihalali au la.

"Hata hivyo, kama hati ya mashtaka ina kasoro isiyoweza kutibika na kesi imeharibika. Ninaona kwamba maslahi ya haki yanataka amri ya kuendesha kesi ya haki dhidi ya mtuhumiwa.

"Ninaelekeza shauri kusikilizwa upya dhidi ya washtakiwa wote wawili mapema iwezekanavyo mbele ya hakimu tofauti.

"Mrufani na mshtakiwa wa pili, Nikolaus Uliza, wataendelea kukaa rumande wakisubiri kesi yao kusikilizwa," alisema.

Jaji Kinyaka alielekeza mwendesha mashtaka abadilishe hati ya mashtaka ili kuashiria kosa la kumiliki vyombo vya kuvunjia nyumba.

# Meli kubwa yenye watalii 2,000 yatia nanga Dar

Na Mary Geofrey

MELI kubwa ya utalii yenye urefu wa mita 294 na uwezo wa kubeba watalii 4,700, imewasili nchini kwa mara ya kwanza kupitia bandari ya Dar es Salaam ikiwa na watalii 2,220 na watoa huduma 1,011.

Meli hiyo, Norwegian Cruise Line (NCL) iliwasili jana saa 12:00 asubuhi, ikitokea Bandari ya Mombasa, Kenya ikiwa ni matokeo ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam ya kuongeza kina na upana wa mlango wa bandari.

Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Mrisho, akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa mapokezi wa meli hiyo, alisema kwa mara ya kwanza Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), imevunja rekodi ya kupokea meli kubwa ya aina hiyo.

Alisema meli hiyo imechukua ukubwa wa gati mbili kuanzia namba mbili hadi tatu ili kushusha watalii kabla ya kuondoka kuelekea nchini Msumbiji, jana.

"Awali meli kama hizi zilikuwa hazifiki kwenye bandari zetu kwa sababu ya kutokuwa na kina kinachotosha kutia nanga. Lakini sasa baada ya maboresho makubwa yanayofanywa na serikali, leo tuna furaha kupokea meli hii kubwa sana ikiwa na watalii wengi ambao wanaenda kwenye vivutio mbalimbali vya utalii nchini," alisema Mrisho.

Aliahidi kuwa huo ni mwanzo wa meli nyingine kubwa kuwasili kwenye bandari hiyo kutokana na kina kirefu cha kuingiza meli yenye urefu wa mita 305.

Alisema mafanikio ya kuwapo kwa meli hizo ni kubeba watu au watalii wengi zaidi kwa wakati mmoja ambayo ni kuongeza Pato la Taifa kupitia utalii pia kushusha mizigo mingi kwa wakati mmoja na kunufaisha wafanyabiashara kwa gharama za chini.

Mkurugenzi wa Huduma za Meli, Uratibu wa Shughuli za Bandari na Nahodha Mkuu wa TPA, Abdallah Mwingamno, alisema maboresho yaliyofanywa na Bandari ya Dar es Salaam ni kuleta meli zenye urefu wa mita 305 hadi 350.

Alisema bandari hiyo inahudumia meli za kontena, mizigo mingine na abiria.

Alisema manahodha walienda Ujerumani kujifunza namna ya kuingiza meli yenye urefu wa mita 305 katika kina cha bandari hiyo.

"Tunaishukuru Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, kazi anayofanya inaonekana na inazaa matunda na usimamamizi wa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasdure Ndossa, kwa kazi kubwa anayofanya," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii, Damas Mfugale, alisema wanajivunia kupokea meli hiyo kubwa yenye watalii wengi ambayo ni zao la kimkakati katika sekta ya utalii.

Alisema wanategemea mwaka mmoja baadaye watongeza idadi ya meli hizo kubwa kuendelea kuingia nchini ambazo zitaongeza idadi kubwa ya watalii wanaotembelea vivutio mbalimbali.

Alisema watalii wengine wanaenda mbuga za wafanyama Selous, Bagamoyo na wengine wataingia kwenye migahawa na sehemu zenye vivutio mbalimbaji mkoani Dar es Salaam.

**HALI BANDARINI**

Mabasi aina ya coastal yalikuwa yakibeba watalii na kuwapeleka maeneo mbalimbali ya utalii kwaajili ya kuangalia vivutio jijini hapo.

Watalii walioshuka kwenye meli hiyo, wengi wao wakiwa wazee na watu wazima, walitembea kwenda kupanda mabasi na wengine wakitembea kutoka bandarini kuelekea maeneo ya Posta mpya.

Wengine wenye ulemavu walikuwa kwenye viti mwendo wakiendeshwa kutembelea maeneo mbalimbali ya bandari hiyo wakifanya mazoezi na kuota jua.

Hali ya biashara ya teksi ilionekana kupamba moto nje ya bandari hiyo watalii wakipanda na kwenda sehemu mbalimbali za mji huo kabla ya kurejea na kuanza tena safari 12:00.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (katikati), akikata utepe kuzindua mitaala itakayotumiwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kufundisha wahudumu wa kwenye mabasi, chuoni hapo jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkuu wa Dawati la Elimu ya Usalama Barabarani wa Jeshi la Polisi, Michaek Deleli (kushoto), Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usafiri wa Barabara (LATRA), Johansen Kahatano (wa pili kushoto) na (wa pili kulia) ni Mkuu wa Chuo cha CBE, Prof. Edda Lwoga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Fundi magari kortini tuhuma kuiba vifaa vya magari vya mil. 148/-

Na Grace Gurisha

FUNDI magari, mfanya usafi na mfanyabiashara wamependishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa na shtaka la wizi wa vifaa mbalimbali vya magari vyenye thamani ya Sh. milioni 148.

Washitakiwa ni Lawrence Lucas (fundi magari), Karim Omary (mfanya usafi) na Ally Said (mfanyabiashara) ambao walisomewa mashitaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya wa mahakama hiyo.

Wakili wa serikali, Cathbert Mbilinyi, alidai kati ya Januari 2022 hadi Februari 2023, mshitakiwa Lucas na Omary waliiba vifaa mbalimbali vya magari vyenye thamani ya Sh. milioni 148.

Alidai kuwa Januari 10, 2023 eneo la Mwembeyanga, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, mshitakiwa Said anadaiwa kukutwa na baadhi ya vifaa vya magari vinavyodaiwa kupatikana kinyume cha sheria, mali ya kampuni hiyo.

Baada ya kusomwa mashitaka hayo, washitakiwa wote walikana. Upande wa mashitaka ulidai, upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kuwasomea washitakiwa hoja za awali na ilipangwa Januari 31, mwaka huu.

Mshitakiwa Lucas na Omary walipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ikiwamo kuwasilisha mahakamani Sh. milioni 74 kila mmoja ama hati ya mali isiyohamishika ya kiasi hicho cha fedha.

Mshitakiwa Said aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la wadhamini wawili waliosaini bondi ya Sh. milioni 74 kila mmoja.

# Kesi ya kujeruhi, kutoa lugha ya matusi kusikilizwa Feb. 19

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam Februari 19, mwaka huu inatarajia kuanza kusikiliza kesi ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi inayowakabili wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54), raia wa India wanaotuhumiwa kwa mashitaka manne.

Kesi hiyo ilitakiwa kuanza kusikilizwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Aaron Lyamuya, lakini ilishindikana kwa sababu hakimu huyo hakuwapo mahakamani kutokana na majukumu mengine.

Wakili wa Serikali, Frank Michael, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo kuwa kesi hiyo iliitwa kwa ajili ya kuanza kusikilizwa na pia wana mashahidi wawili na wapo tayari kuendelea.

"Mheshimiwa tunao mashahidi wawili na tupo tayari kuendelea, lakini tulikuwa tunaomba tarehe nyingine ya usikilizwaji kwa sababu hakimu anayesikiliza kesi hii hayupo," alidai Wakili Michael.

Hakimu Kiswaga aliwaonya mashahidi hao na kuwataka kufika mahakamani hapo Februari 19 kwa ajili ya kutoa ushahidi wao.

"Mashahidi nawaonya kufika tarehe hiyo na huyo shahidi ambaye amesema tarehe hiyo hatakuwapo atawasiliana na wakili wa serikali, atatoa ushahidi wake kwa njia ya mtandao 'Video Conference' kwa sababu vifaa vipo," alidai.

Kwa mujibu wa hati ya mashitaka, washitakiwa hao wanaoishi Mrina - Kisutu, jijini Dar es Salaam wanaotuhumiwa kuyatenda Julai 21, 2023.

Katika shitaka la kwanza la kujeruhi linalomkabili Nathwan, anatuhumiwa Julai 21, 2023 akiwa eneo la Mrina-Kisutu, Wilaya ya Ilala, kinyume cha sheria alimsababishia madhara makubwa Kiram Abdallah kwa kuzamisha kichwa chake kwenye chokaa.

Pia, katika shitaka la pili la shambulio la mwili linalomkabili Nathwan, tarehe hiyo na eneo hilo alimsababishia madhara Lalit Kanabar katika mwili wake kwa kumpiga ngumi na mateke kichwani.

Ilidaiwa kuwa katika shitaka la tatu na la nne linalomkabili Sangita, anatuhumiwa kutoa matusi makubwa dhidi ya Abdallah na Kanabar kitendo kilicholeta fujo kwa namna ambayo inaweza kuleta uvunjifu wa amani.



## DCEA yazipiga msasa asasi za kiraia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imetoa mafunzo kwa asasi za kiraia zinazotoa huduma kwa waraibu ya uandishi wa andiko la miradi kwa ajili ya kuwasaidia kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Katibu Tawala Msaidizi, anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji Mali, Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha, Hargeney Chitukuro alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa asasi hizo ili kutoa elimu zaidi na matibabu kwa waraibu hao na umakini wa matumizi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kudhibiti matumizi ya dawa hizo nchini.

Alisema uandishi wa maandiko ya miradi ni muhimu kuzingatia ili kusaidia serikali katika mapambano ya matumizi ya dawa hizo kuibua miradi mbalimbali, ikiwemo utoaji wa elimu kwa jamii kuanzia shuleni, vyuoni, taasisi za fedha na maeneo mengine.

Awali Ofisa Maendeleo ya Jamii wa DCEA, Kanda ya Kaskazini, Sarah Ndaba alisema elimu hiyo ya uandishi wa andiko ni muhimu kusaidia wadau kusaidia jamii kupata elimu sanjari na ufanyaji kazi kwa ufanisi zaidi kwa lengo la kuisaidia serikali kwenye mapambano hayo.

Alisema mamlaka hiyo ina asasi zaidi ya 100 na kwa Kanda ya Kaskazini wanaoshirikiana na asasi zaidi ya 16 ambazo zinatoa mrejesho juu ya udhibiti wa dawa hizo, sanjari na urejesho kwa mamlaka ya DCEA juu ya mchanganuo wa kazi wanazofanya au walizofanya kwa kila mwaka.

"Lazima tuwe weledi katika uandishi wa maandiko yao ili kupata uelewa na mbinu mpya ya maandiko bora ya kushawishi wafadhili, kutoa fedha kwa ajili ya mapambano hayo nchini kwani asasi za kiraia zina umuhimu mkubwa wa kupambana na dawa hizo ikiwemo utoaji elimu kwa jamii, " alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hao kutoka mkoani Tanga wa Shirika la Gift of Hope Foundation, Said Bandawe, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao kwani yatawasaidia kupata fedha na kufanya harambee kukusanya fedha kwa ajili ya kusaidia kudhibiti dawa hizo na kutoa elimu kwa jamii.

Ofisa Elimu kutoka DCEA, Shabani Miraji alisema mamlaka hiyo itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali nchini kudhibiti dawa hizo, kutoa elimu zaidi na kubaini mbinu za kudhibiti mbinu mpya wanazotumia wafanyabiashara wa dawa hizo.

# Wananchi 'wamng'oa' mkandarasi wa taka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKAZI wa Kata ya Murieti katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, wamemkataa mzabuni wa kukusanya taka na kuitaka serikali kuvunja mkataba kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya mkataba.

Mzabuni huyo anadaiwa kushindwa kupita mitaani kuzoa taka mara moja kwa wiki na badala yake anafanya hivyo kwa mwezi na kuhatarisha afya za wakazi wa kata hiyo.

Kwa nyakati tofauti jana, wakazi hao waliwasilisha kilio chao kwa wajumbe wa Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arusha, iliyotembelea eneo hilo, ikiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya, Timoth Sanga.

Mkazi wa Murieti, Lilian Daudi alisema: "Tupo hatarini kupata magonjwa ya mlipuko, taka zimejaa, zimezagaa mtaani. Mwezi mzima sasa, hatuoni gari la taka, hasa ukizingatia huu ni msimu wa mvua.

"Yaani taka zinaoza na mzabuni aliyepewa kazi haonekani na mvua zinazoendelea kunyesha taka zinaoza na watoto wetu ni wadogo. Ikiwezekana mkataba uvunjwe kwa sababu tunashindwa kuwazuia watoto wasishike taka, wakati wa kucheza au tunawapowatuma dukani na maeneo mengine."

Ofisa Afya wa Kata hiyo, Frank Njiku, alipotakiwa kuwajibu wakazi hao kuhusu malalamiko yao, alisema ni kweli wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na mlundikano wa taka kwa muda mrefu.

"Mzabuni wa awali aliondolewa kutokana na uzembe wa kushindwa kutekeleza majukumu yake, lakini kwa sasa hata huyu mzabuni mpya anashindwa kufanya kazi kutokana na kutolipwa kwa wakati. Hajalipwa kwa sababu mfumo wa malipo wa Halmashauri ya Jiji, una tatizo.

"Huu uchafu na majani yalioyojaa kwenye baadhi ya mitaro, naomba niahidi kwamba nitawasiliana na watendaji wa mitaa yote 13 ya Kata ya Murieti ili wasimamie usafi katika maeneo yao."

Sanga aliwaahidi kuwa atarejea katika kata hiyo kabla ya kumalizika kwa Januari mwaka huu na atahakikisha mzabuni huyo anatekeleza majukumu yake kwa wakati.



Mkufunzi Mwandamizi Elekezi wa Jeshi la Wanamaji na Mkuu wa msafara wa wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi, Treseas Rutambuka (wa pili kulia), akikabidhi ngao kwa Kaimu Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Kisare Makore mjini Moshi juzi, kama alama ya kumbukumbu ya wanafunzi 12 wa chuo hicho kutoka nchi saba duniani waliofika mkoani humo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. **PICHA: MARY MOSHA**

# Wanafunzi NDC wapatiwa mafunzo ya usalama

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAOFISA 12 kutoka mataifa sita ya Bara la Afrika ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) wameanza mafunzo ya vitendo katika mikoa ya Kilimanjaro na Manyara ya ushauri kuhusu usalama, chakula, mazingira, kilimo, uwekezaji na utalii.

Mkufunzi Mwandamizi Elekezi wa Kikosi cha Wanamaji na kiongozi wa msafara wa wanafunzi hao kwa Kanda ya Kaskazini, Commodore, Traseas Rutambuka, alisema watakuwa Mkoa wa Kilimanjaro kwa siku tano kutembelea maeneo mbalimbali.


"Usalama sio jeshi tu bali umejikita katika chakula, mazingira, kilimo, uwekezaji na utalii. Hapa tumeongozana na maofisa wanafunzi kutoka mataifa ya Misri na Nigeria na sita kutoka Tanzania.

"Kozi hii ni ya wiki 47, na ina wanafunzi 53 kutoka nchi 17. Wote hao hujifunza darasani na kila mwisho wa muhula, huenda kujifunza kwa vitendo katika mikoa mbalimbali na kujionea hali halisi.Huwa tuna nafasi ya kushauri kwa usalama wa taifa."

Akizungumza katika kikao cha utambulisho, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Vedast Makota, alisema serikali itawapa ushirikiano wa kutosha kujifunza hali uchumi na uzalishaji wa chakula.

"Tumewaonyesha hali halisi ya kiuchumi, biashara katika mkoa ipo katika kiwango gani. Lengo ni kuwafanya waweze kuelewa mkoa husika, pia tumezungumza hali ya kisasa," alisema Dk. Makota.

Baadhi ya washiriki, akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Rombo, Godwine Chacha alisema ujio wao utawasaidia kujifunza kuhusu dhana nzima ya uwajibikaji.





# ‘Marufuku kuuza chakula shuleni’

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga imepiga marufuku uuzaji chakula shuleni ili kuwanusuru wanafunzi kukumbwa na ugonjwa wa kipindupindu.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi CCM Wilaya ya Shinyanga.

Kwa mujibu wa Johari, kipindupindu kipo hivyo ili kukabiliana nacho lazima kuchukua tahadhari, ikiwamo kupiga marufuku uuzaji wa chakula shuleni ili kulinda afya za watoto, wananchi kufanya usafi wa mazingira na kunawa mikono kwa sabuni kabla na baada ya kula chakula.

“Ni marufuku kwa sasa kufanya biashara ya kuuza chakula shuleni, hali ni mbaya ugonjwa wa kipindupindu upo,” alisema.

Aliwataka wananchi wachukue tahadhari kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa wilaya amewasihi madiwani na viongozi kuhamasisha wazazi kupeleka watoto shule wakapate elimu na kutimiza ndoto za kuwa viongozi wa baadaye wa taifa.

“Rais wetu ametoa fedha nyingi za kujenga shule ili watoto wote wasome bure, hivyo tuhimizane watoto wote waliofaulu na wanaostahili kuandikishwa waende shule hata kama hawana sare,” alisema Johari.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko alionyesha kusikitishwa na mwitikio mdogo wa wazazi kupeleka watoto wao shule.

Masumbuko alitoa mfano wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga kuwa wanafunzi 361 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 361 mwaka huu, waliochukua fomu 266, kati ya hao walioripoti shule ni 132.



Wapita njia wakivuka maji yaliyojaa barabarani katika Kijiji cha Kisai, wilayani Urambo, mkoani Tabora juzi, kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC akagua chemba MWAUWASA

**Thomas Wandiba,** SAUT

MKUU wa Wilaya ya Ilemela mkoani hapa, Hassan Masala ameiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kukarabati chemba za maji taka ili kuwakinga wananchi kukumbwa na kipindupindu.

Masala alitoa agizo hilo baada ya Wakazi wa Mtaa wa Magomeni Kata ya Kirumba kulalamikia ubovu wa chemba za vyoo kuwa unahatarisha maisha yao kutokana na maji taka kusambaa kwenye makazi yao.

Akizungumza katika mtaa huo baada ya kutembelea maeneo hayo Masala alithibisha ukubwa wa tatizo hilo na kuiagiza MWAUWASA kufanya maboresho ya miundombinu hiyo ili kuwakinga wananchi na kipindupindu.

“Tukubaliane kipindipindu ni uchafu, hivyo niwaombe mamlaka kutatua kero hii haraka iwezekanavyo, hatuna budi kuweka mazingira yetu katika hali safi na salama,” alisema.

Aliwaonya wananchi kuacha tabia ya kufungulia vyoo wakati mvua zinaponyesha kwa kuwa wanachangia kuenea kwa magonjwa ikiwemo kipindupindu.

Jana Nipashe liliripoti malalamiko ya wakazi hao kuwa chemba hizo zinahatarisha maisha yao kutokana na kutiririsha majitaka kwenye makazi yao na kuwa hatarini kuugua kipindupindu.

Walidai kuwa chemba hizo zimechakaa na baadhi ya mabomba kupasuka hivyo kutiririsha majitaka kwenye makazi yao na kuhatarisha afya zao na watoto kwa kuchezea.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Magomeni Abdallah Hega alikaririwa na gazeti hili jana akisema kuwa ameandika barua MWAUWASA kulalamikia tatizo hilo.

Hega alisema baada ya kupokea barua hiyo waliahidi kuwa wangefika kwenye maeneo yao na kurekebisha kwa kufunga mashine nyingine mpya, lakini mpaka sasa hawajafanya hivyo.

Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira MWAUWASA, Salim Lossindilo, alisema mamlaka hiyo imesaini mkataba Novemba 23, mwaka juzi wenye thamani ya Shilingi bilioni 12.7 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya maji taka katika maeneo ya Ilemela na Jiji la Mwanza.

“Kwa sasa kazi ya kuhuisha usanifu wa mradi inaendelea na itakapokamilika taratibu za manunuzi ya mkandarasi zitafanyika ikiwa matarajio ni kuanza kazi za ujenzi mapema mwaka huu na kukamilika Mwaka 2026,” alisema na kusisitiza kuwa: “Baada ya kukamilika tuna imani kuwa tatizo hili litakuwa limedhibitiwa kwa asilimia 100.” .

## Mgodini wahofia kipindupindu

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

UONGOZI wa mgodi wa dhahabu wa Nyakafuru wilayani hapa Mkoa wa Geita umeombwa kuboresha usafi wa mazingira kwenye eneo la uchimbaji, makazi na kuwa na vyoo bora ili kudhibiti mlipuko wa kipindupindu mgodini.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wachimbaji wa madini hayo katika mgodi huo wakati wakizungumza na Nipashe wanavyoendelea kuchukua tahadhari ya kukabiliana na kipindupindu baada ya kuikumba baadhi ya mikoa ya kanda ya ziwa kutokana na uchafu.

Mchimbaji Pili Mahona, alisema uongozi wa mgodi kwa kushirikiana na wataalamu wa afya kutoka halmashauri ni kuwapatia elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Mwenyekiti wa mgodi huo, Vicent Maige alisema wanaendelea kuwaelimisha wananchi, wachimbaji, mamalishe kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema jukumu walilonalo ni kuhamasisha wachimbaji hao na jamii kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono wanapotoka chooni na kabla ya kula.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, Dk. Zakayo Sungura aliwataka wachimbaji hao kuacha tabia ya kujisaidia vichakani, kuchemsha maji ya kunywa na kunawa mikono.

Dk. Sungura alisema wamefunga vilabu vya pombe za kienyeji na biashara ya juisi ya miwa kutokana na mazingira kutoridhisha.

Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Sakina Mohamed alisema ametoa maelekezo kwa wenyeviti wa wachimbaji hao kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Sakina alisema amekutana na watendaji wa serikali na kuwaagiza kufikisha ujumbe kwa wananchi kuhakikisha wanazingatia kanuni za afya na matumizi sahihi ya vyoo.

**Alisema jukumu walilonalo ni kuhamasisha wachimbaji hao na jamii kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono wanapotoka chooni na kabla ya kula.**



Ukurasa 12

**UN na sheria zinazoboreshwa, yaibua kikwazo kufikia 50/50**





Ukurasa 13

Wanawake wanavyochomoza katika uongozi Zanzibar


# siasa

JUMATANO JANUARI 17, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**‘KELELE ZA CHURA’ DRC**

**Hazimzuii Tshisekedi kuapa, ni Jumamosi**

## NCHIMBI APEWA `HOMEWORK’

# Umo mgawo umeme unaozidi kutikisa, katiba mpya ya wananchi, bima ya afya

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya CCM kumtangaza Dk. Emmanuel Nchimbi, kuwa Katibu Mkuu wa chama, nahodha huyo anashika usukani wakati Watanzania wakikabiliwa na kero nyingi, licha ya kwamba chama chake kinamtegemea kukivusha kwenye uchaguzi.

Baadhi ya wasomi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, wanaozungumzia uteuzi wake wanaiambia Nipashe kuwa, anawajibika kuongeza uwazi ndani ya uchaguzi wa serikali za mitaa na kuondoa kasoro ambazo zinalalamikiwa za kuubeza upinzani.

Wanasema Dk. Nchimbi amechaguliwa kuongoza CCM wakati ambao macho na masikio ya serikali yakielekezwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na ule Mkuu wa 2025, hali inayoashiria kwamba hakuna anayeangalia maisha baada ya uchaguzi.

Hata hivyo, Dk. Nchimbi Mtendaji Mkuu wa chama tawala pamoja na kuhakikisha kwamba anajenga imani ya wananchi kwa chama na serikali, mambo yanayowakwaza Watanzania ni mengi ikiwa ni pamoja na kukatika kwa umeme mara kwa mara, mustakabali wa kuwapo kwa bima ya afya na tatizo la ubadhirifu wa fedha za umma.

Wanasema licha ya kwamba chama anachokiongoza kinaelekeza masikio na macho kwenye mchakato na matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa ili kujua hatima na kujipanga kwa ajili ya uchaguzi mkuu, ni lazima kuongeza uwazi, uwajibikaji na uhuru kwenye kupata uwakilishi bungeni na kwenye kata.

Wasomi hao wanasema Watanzania wanafahamu na wanaelewa kinachoendelea kisiasa na wanatamani kuwa na uwakilishi ambao uwajibika kwao na kuisimamia zaidi serikali ili kupunguza ugumu wa maisha.

Wakizungumzia baadhi ya changamoto ambazo wanataka zifanyiwe kazi wanataja nishati wakiliita jambo sugu ambalo wananchi wanalalamikia, hasa kukatika umeme.

Wanahoji inakuwaje tatizo linaongezeka wakati kuna miaka hakukuwa na mgawo? Waliotangulia walifanya nini na sasa shida iko wapi?

Wanamshauri Katibu Mkuu atumie mbinu na juhudi zote kumaliza shida hiyo kwa kuielekeza serikali kutoa maelezo mara kwa mara kuhusu utatuzi wa changamoto hiyo.

Kisiasa suala la Katiba Mpya na Tume huru ya uchaguzi ni mambo ambayo ni madai ya wananchi, wadau wa siasa na hata wanaofuatilia mwenendo wa kisiasa waliopo nje ya mipaka ya Tanzania.

Miongoni mwa wadau hao ni viongozi wa dini, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Viongozi wa Dini, Askofu William Mwamalanga, akitoa maoni yao, anasema madai ya katiba mpya hayajaanza leo akikumbushia Tume ya Jaji Francis Nyalali ya miaka ya 1990.

“Katiba mpya imechukua miaka mingi kupatikana na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema siyo tena suala la mjadala. Amewapa Watanzania matumaini ya kuipata. Tunategemea Dk. Nchimbi ataikumbusha serikali kutekeleza ahadi zake na hasa kuandaa katiba mpya,” anasema.

Askofu Mwamalanga anasema mtendaji huyo mpya anaijua hali ya nchi, Watanzania pamoja na mienendo ya kidemokrasia akimtaka asimamie kupatikana kwa katiba ya wananchi, kukomesha ubadhirifu serikali na kuondoa migogoro ya kisiasa.



Katibu Mkuu, Dk. Emmanuel Nchimbi, baada ya kuteuliwa na Kikao Maalum cha Halmashauri Kuu, Jumatatu wiki hii huko Zanzibar. **PICHA: CCM**

Anataja mgogoro wa mazungumzo ya maridhiano baina ya CCM na CHADEMA ambayo yamekwama na sasa chama hicho cha upinzani kimetangaza kufanya maandamano nchi nzima, hali inayoongeza wasiwasi.

Kuhusu ubadhirifu wa fedha za umma anasema: “Tunataka kuona wale waliotajwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Umma (CAG), wanawajibishwa kwa kushtakiwa na hatua za kudhibiti mifumo ya kuvuja na kuibiwa fedha za walipakodi zinachukuliwa.”

“Naweza kusema kazi kubwa aliyonayo ni kuleta mabadiliko kama ataweza ya kukubali kuandika Katiba ya wananchi, tume huru na kukomesha wizi serikali...haya yatajenga imani ya chama chake kwa Watanzania,” anafafanua Askofu Mwamalanga.

Mmoja wa wadau wa afya kutoka sekta binafsi akizungumzia uteuzi wa Dk. Nchimbi, anasema ni wakati wa kutoa majibu ya mkwamo wa bima ya afya akirejea bima ya watoto maarufu kama Toto afya kadi.’

“Inavyoelekea haijafahamika kuwa watoto wengi wanapoteza maisha kwa kukosa matibabu baada ya bima yao kufutwa, hili ni jambo ambalo wapigakura wana hamu ya kulisikia kutoka serikalini,” anasema.

Mwekezaji huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, anasema suala la afya ni tatizo linalohitaji ufumbuzi wa haraka badala ya taarifa za mafanikio ya ujenzi wa vituo vya afya ambavyo hawana uhakika wa kutibiwa huko.

Wachambuzi wa masuala ya siasa wanaona uzoefu wa Dk. Nchimbi ndani ya chama, serikali na kwenye anga za kimataifa, ni karata muhimu ya kuivusha CCM kwenye maeneo mengi ikiwa atautumia vizuri.

“Anakijua chama vizuri, amekuwa serikali na ni balozi. Ni mtu muhimu tuliyemhitaji wakati huu hasa tunapoelekea kwenye chaguzi,” anasema Kamishna wa zamani wa Madini, Dk. Peter Kafumu.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Repoa ya jijini Dar es Salaam, Profesa Donald Mmari, anasema Dk. Nchimbi ni mtu anayeelewa mahitaji ya nchi na chama na akigusia dhana ya diplomasia ya uchumi.

“Ni mwanadiplomasia kwa hiyo anafahamu nchi inahitaji nini, mahusiano ya kimataifa, tunapozungumzia dhana ya diplomasia ya kiuchumi kwa hiyo anaweza kukisaidia chama katika kuielekeza na kuishauri serikali namna bora ya kusimamia mageuzi ya kiuchumi na kujenga mahusiano,” anasema.

Dk. Nchimbi anachukua kijiti kutoka kwa Daniel Chongolo, aliyejiuzulu Novemba mwaka jana na Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, kuridhia maombi yake.

# UN na sheria zinazoboreshwa, yaibua kikwazo kufikia 50/50

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN Women), ni mdau wa maendeleo ya kinamama katika siasa na uongozi, ili kufanikisha azma hiyo, linaguswa na kutoa maoni kwenye mchakato wa kuboresha sheria ili kuweka mazingira bora ya uchaguzi wenye mrengo wa usawa kijinsia.

Maoni yake yanaelekezwa kwenye sheria zinazoboreshwa ili kuwa na uchaguzi huru, haki na unaokubalika za uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa.

UN Women inaangazia upungufu katika sheria hizo na jinsi zinavyorudisha nyuma juhudi za mwanamke kufikia uwakilishi wa asilimia 50 kwa 50 kwa mrengo wa kijinsia.

UN Women kwa kushirikiana na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Kikundi cha Mawasiliano cha Umoja wa Mataifa, wanafanya mkutano na Jukwaa la Wahariri kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa kijinsia wa miswada hiyo na kutoa mapendekezo ili kuwapo uwiano na ushiriki wa wanawake na wanaume kwa kiwango cha 50/50 katika michakato ya kisiasa.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwakilishi Mkazi UN Women, Hodan Addou, anasema katika awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suhuhu Hassan, Tanzania imepiga hatua kubwa kufikia ongezeko kubwa la wanawake kushiriki siasa na nyadhifa za juu uongozini.

"Tanzania wanawake wanawakilishwa bungeni kwa asilimia 37.4 na kwenye viti maalum tuna uwakilishi kwa asilimia 30 pamoja na kuwa na wanawake katika wizara muhimu," anasema.

Anaongeza kuwa licha ya juhudi hizo taifa liko nyuma ya makubaliano ya mikataba ya kimataifa iliyosaini inayoelekeza nchi wanachama kuchukua jitihada za makusudi za kisheria na kisera kufikia uwiano wa 50:50 kwa wanawake na wanaume kiuongozi.

Moja ya mikataba hiyo ni wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu juu ya Haki za Wanawake barani Afrika (Maputo Protocol) unaowataka wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), kufikia uwiano huo ifikapo mwaka 2015.

Anasema nafasi hizo ni muhimu kwa wanawake, kwa kuwa wanashiriki katika kutungwa sera na sera na kutoa maamuzi muhimu ambayo yanaathiri maisha yao katika ngazi ya jamii.

Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Zlatan Milisic, anasema kwanza uwakilishi mdogo wa wanawake kwenye kufanya maamuzi unatokana na sababu mbalimbali ikiwamo upungufu wa kijinsia katika sheria na sera.



Mwakilishi Mkazi UN Women, Hodan Addou na Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Zlatan Milisic, wakizungumza na wana habari. **PICHA: JENIFER GILLA**

> Tanzania wanawake wanawakilishwa bungeni kwa asilimia 37.4 na kwenye viti maalum tuna uwakilishi kwa asilimia 30 pamoja na kuwa na wanawake katika wizara muhimu.

Aidha, anataja kukosa uwezo na ujuzi muhimu kati ya wanawake, unyanyasaji katika siasa, mitazamo ya kijinsia, desturi za kitamaduni, mitazamo na kanuni kuwa pia hukwamisha.

Anagusia pia ukosefu wa usawa sio tu kuwa unadhoofisha kanuni za uwakilishi wa kidemokrasia, lakini pia unazuia maendeleo ya nchi na UN inashirikiana na serikali iliyopo madarakani kuhakikisha wanawake wanashiriki katika nafasi hizo.

"Mfumo wetu wa Ushirikiano Endelevu wa Umoja wa Mataifa kwa Tanzania 2020 hadi 2027 pia unatambua kwamba ushirikishaji wanawake katika siasa ni muhimu kufikia maendeleo endelevu na pia kushughulikia masuala yanayowaathiri kinamama na wasichana," anaongeza.

Akiwasilisha uchambuzi huo, Mhadhiri wa Sheria wa Chuo Kikuu Huria Tanzania, Dk. Victoria Lihiru, anaeleza kuwa wamegundua changamoto nane anazokumbana nazo mwanamke katika harakati za kushiriki siasa na uongozi zinazotokana na upungufu kisheria.

Idadi ndogo na ushiriki hafifu wa wanawake kama viongozi ndani ya vyama vya siasa ni changamoto ya kwanza.

Idadi ndogo ya wanawake wagombea na wanaochaguliwa katika nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na serikali kuu nayo ni changamoto anayogusia Victoria.

Nyingine ni zile zinazowakumba wanawake viti maalumu, madiwani na wabunge, akisema idadi ndogo ya makamishna, viongozi na wafanyakazi kwenye Tume za Taifa za Uchaguzi na mchakato wote wa uchaguzi na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika siasa.

Victoria anataja pia uhaba wa fedha kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika siasa na uchaguzi.

Utatuzi wa migogoro usiofuata kanuni za asili za kutoa haki ndani ya vyama vya siasa, kutokuwapo taarifa zinazohusu uchaguzi na siasa zilizochakatwa kwa misingi ya kijinsia na ujumuishwaji wa makundi maalumu nayo ni changamoto.

"Zimesababisha kuwapo na idadi ndogo ya wanawake wanaoteuliwa kama wagombea wa nafasi za uongozi wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa mwaka 1995 huku wengi wakitegemea zaidi viti maalumu kuufikia ubunge na udiwani."

"Katika bunge lenye wabunge takribani 400, wanawake wabunge ni asilimia 37.2 au 148. Kati yao ni 27 pekee sawa na asilimia 10.4 ndiyo wamechaguliwa katika majimbo 264. Idadi kubwa ambayo ni wabunge 113 wameingia kupitia viti maalumu."

Kati ya madiwani takribani 4,000, ni asilima 6.5 pekee ya madiwani wanawake waliochaguliwa kutoka kwenye kata," anasema.

### MAPENDEKEZO

Kwa mujibu wa Dk. Victoria baadhi ya mapendekezo ni vifungu 6A(5) 10C vya sheria ya vyama vya siasa vifanyiwe marekebisho kuweka asilimia na viwango vya ujumuishwaji wa wanawake na makundi maalumu katika vyama hususani katika kuchagua viongozi wake pamoja na wajumbe wa vyombo na mikutano ya maamuzi.

Aidha, kifungu cha 32 cha Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kiongezewe kifungu kidogo kitakachovitaka vyama kama vikiteua mgombea urais mwanamume makamu wake awe mwanamke au akiwa mwanamke makamu awe mwanaume.

Anongeza kuwa vifungu 4(5) (c), 13, 16, 17 na18 vya Sheria ya Vyama vya Siasa vibadilishwe kutaka ruzuku ya asilimia 30 kutolewa kwa vyama kulingana na namna chama kitakavyotekeleza sera na mipango inayozingatia ujumuishwaji wa wanawake na makundi maalumu katika nafasi za uongozi, maamuzi na kuteua wagombea wa chaguzi za serikali.

Kadhalika, vyama vya siasa vionyeshe namna vinavyotumia fedha za ruzuku kutoka wadau mbalimbali kukuza ushiriki wa wanawake na makundi ya kijami katika michakato ya siasa.

"Chama kisipewe ruzuku ya asilimia 30 kama hakina mikakati ya kukuza ushiriki wa makundi ya kijamii katika michakato ya siasa," alisema.

Aidha, vifungu cha 9 (6) (8) vya Sheria ya Uchaguzi vielekeze kamati ya uteuzi kuhakikisha inazingatia usawa wa jinsia, ujumuishwaji wa makundi maalumu katika kuwapata wajumbe tisa wa tume wanaopendekezwa ili kuwapo na usawa wa jinsia wa wajumbe wateule, ni pendekezo jingine.

Anasema matarajio ya wadau wa haki za binadamu na haki za wanawake na usawa wa jinsia ni kuwa miswada hiyo itasaidia kutatua baadhi ya changamoto zinazosababisha ushiriki mdogo wanawake na kinamama wenye ulemavu kwenye uchaguzi.

# Wanawake wanavyochomoza katika uongozi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

USAWA wa kijinsia ni wimbo ambao umekuwa na mwangwi kila kona ya dunia. Hiyo ni kutokana na vuguvugu lililopata mashiko kutaka kuwe na uwiano sasa kati ya wanawake na wanaume kwenye vyombo vya uamuzi kama vile bunge, baraza la wawakilishi, baraza la mawaziri, uongozi wa taasisi za umma na mashirika.

Lengo kubwa la suala hili ni kuwa na uwakilishi wa 50 kwa 50 baina ya wanawake na wanaume katika ngazi za uamuzi. Mvumo huu sasa uko katika jumuiya za kikanda kama Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Afrika (AU).

Tangu kuanza kwa vuguvugu hilo miaka 2000 mwanzoni, kumekuwa na kasi katika uteuzi au uchaguzi wa wanawake kuingia katika masuala ya uongozi. Zanzibar ambayo wiki iliyopita ilikuwa inatimiza miaka 60 ya Mapinduzi, ajenda mojawapo tangu mwaka 1964 ilikuwa kuondoa ubaguzi wa kijinsia hasa katika nafasi za uongozi na ushiriki wa katika kisiasa kati ya wanawake na wanaume.

Ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi, Zanzibar ni tofauti na ilivyokuwa mwaka 1964. Baraza la Mapinduzi la mwaka 1964 lilikuwa na wajumbe 10 wote wakiwa wanaume. Kwa sasa mambo yamebadilika na wanawake wanachomoza katika vyombo vya uamuzi na kuongeza ushiriki katika ungozi. Kwa sasa serikali ya awamu ya nane chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ina mawaziri 20 wakiwamo watano wanawake.

Aidha, katika Baraza la Wawakilishi la sasa, kuna wajumbe 78 wakiwamo wanawake 29 wakiwamo ambao waliochaguliwa majimbo 50 ya uchaguzi Zanzibar ni nane.

Mwanasiasa mkongwe mwanamke, Balozi Amina Salum Ali, anasema uwapo wa Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ni kielelezo cha mafanikio kwa wanawake katika nafasi za juu za uongozi. Anasema jambo hilo lilikuwa nadra sana katika miaka kadhaa iliyopita.

Balozi Amina ambaye amewahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi serikalini na katika taasisi za kimataifa, anasema hivi sasa kuna nafasi nyingi za uongozi kwa wanawake licha ya kwamba mwaka 1964 walipewa nguvu na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, kufanya biashara ili kujikomboa kiuchumi.

Anasema baada ya Mapinduzi, wakati wa uongozi wa awamu ya pili chini ya Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi, wanawake walipewa nafasi za uongozi zikiwamo za uwaziri.



Amina Salum Ali



Zena Ahmed Said

Kwa mujibu wa Balozi Amina, kila awamu ya serikali inapoingia madarakani, idadi ya ushiriki wa wanawake huongezeka. Anasema kama ilivyokuwa kwa Jumbe, pia wakati wa awamu ya tano chini ya Dk. Salmin Amour Juma, pia wanawake walipewa nafasi katika wizara nyeti wakiwamo makatibu wakuu.

"Kipindi cha Dk. Salmin, nilikuwa mwanamke wa kwanza kuongoza wizara nyeti ya fedha. Pia mawaziri waliofuatia, awamu ya sita na ya saba, wanawake walipewa nafasi," anasema.

Balozi Amina ambaye katika kinyang'anyiro uteuzi wa mgombea urais wa Tanzania ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2015 na ule wa Zanzibar mwaka 2000, anasema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inawapa nafasi za uongozi zikiwamo ukuu wa mkoa na kwa sasa kati ya mikoa mitano yuko mwanamke, Salama Mbarouk Khatib.

Pia katika ngazi ya mahakama, anasema kuna majaji wanawake watano na mahakamani wakazi wanawake 21. Licha ya nafasi hizo, kwa sasa Zanzibar ina Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said.

Dk. Mzuri Issa, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, anasema kuna mabadiliko chanya ya uongozi kwa wanawake kwa sababu miaka ya 1964 ushiriki wa wanawake ulikuwa mdogo.

Anasema mwaka 1867 kulikuwa na mwanamke aliyeshiriki baraza la uamuzi la masuala ya sheria, Kristina Majaliwa, ambaye hata hivyo hakuwa na uamuzi kwa sababu yalipoibuka masuala ya wanawake, haruhisiwi kupiga kura.



Salama Mbarouk Khatib

Pia anasema kipindi hicho kulikuwa na hofu kubwa dhidi ya wanawake pamoja na mifumo dume kwa kutowahusisha katika uongozi. Lakini wanawake wengi walikuwa hawapelekwi shuleni kupata elimu, jambo ambalo ni sababu ya wanawake kuachwa nyuma.

Dk. Mzuri anasema miaka ya 1970, kuwapo kwa uhamasishaji wa wanawake kupata elimu na mwaka 1985, ulipatikana msukumo mkubwa wa haki za wanawake na majadiliano yakaanza na hatimaye kushirikishwa katika harakati za uongozi.

> Kwa kweli wanawake niliowateua hawajiangusha wanafanya kazi vizuri mno na nasema sitasita kuwachagua kunisaidia katika majukumu ya kazi zangu katika kuliongoza taifa.

Anasema mwaka 1985 vilianzishwa viti maalum katika vyombo vya uamuzi na asilimia 10 iliwekwa kwa kwenye Baraza la Wawakilishi na mpaka kufikia asilimia 42 kwa sasa lakini kuundwa kwa wizara ya masuala ya jinsia mwaka 1990.

Wanawake hivi sasa, anasema wanapewa nafasi za uteuzi na wanafanya vizuri wanapopewa na ni waaminifu katika utendaji kazi kwa kuwa si wengi wanaotuhumiwa na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

Pia anasema kwa sasa wanawake wenye elimu na wenye uwezo wa kitaalamu ni wengi, hivyo kuna haja ya kuwapo kwa uchambuzi wa kijinsia kwa kila sekta na serikali kutoa ripoti ya mwaka ya hali ya kijinsia katika nchi.

Anasema pamoja na kuwapo wanawake katika uongozi, bado kuna nafasi za kitaaluma wanawake wameachwa nyuma zikiwamo nishati, ujenzi, uvuvi, sekta binafsi na umiliki wa biashara kutokana na kipato kuwa kidogo.

Kwa mujibu wa Dk. Mzuri katika miaka 60 ya Mapinduzi, jambo la kujivunia ni kwamba wanawake wanaungana na sauti zao zinasikika tofauti na miaka ya nyuma walipokuwa waoga wa kuzungumza. Anasema kwa sasa wanazungumza na kudai haki pale wanaponyimwa.

"Wanawake sasa wamekuwa na ujasiri mkubwa kwa sababu wamekuwa shupavu wa kutojali wale wanaorudisha nyuma harakati za kujikomboa. Hivi sasa sauti za wanawake ni kubwa," anasema.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, anasema katika miaka 60 ya Mapinduzi, ushiriki wa wanawake katika harakati za kisiasa, kiuchumi na kijamii ni mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Anasema serikali inatoa kipaumbele ya elimu kwa watu wote bila kujali jinsia hali ambayo imesababisha watoto wa kike kufanya vizuri zaidi katika mitihani ya taifa.

Pia anasema wanawake wanashirikiana katika harakati mbalimbali za kujipatia kipato ili wasiachwe nyuma kimaisha.

Rais Dk. Mwinyi anahanikiza kuwapo kwa nafasi zaidi za wanawake katika vyombo vya uamuzi kwa kuahidi kuwa hatasita kuwapa nafasi za uongozi wanawake katika serikali yake kwa sababu anaridhishwa na utendaji wa kazi kwa wale aliowapa nafasi.

"Kwa kweli wanawake niliowateua hawajiangusha wanafanya kazi vizuri mno na nasema sitasita kuwachagua kunisaidia katika majukumu ya kazi zangu katika kuliongoza taifa," anasema.

# Kelele za chura DRC; hazimzuii Tshisekedi kuapa, ni Jumamosi hii

• Hofu, upinzani vyaanza kwa washirika wake

**Na Moshi Lusonzo**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, wakati wowote kuanzia sasa anajiandaa kuapishwa na kuunda serikali yake baada ya muungano wa vyama vinavyotawala nchi hiyo kupata viti vingi katika uchaguzi wa wabunge na rais.

Muungano huo unaoundwa na vyama tofauti vya siasa unaojulikana kama Union Sacree, ambao umejipatia kura nyingi kuliko ilivyotegemewa na sasa umejihakikishia kuongoza kwa muhula wa pili baada ya kushinda viti zaidi ya 400 kati ya 500 vya wabunge kwenye uchaguzi uliofanyika Desemba 20, mwaka jana.

Changamoto kubwa katika kuunda serikali zitatokana na ugawanaji ulio sawa wa madaraka ndani ya taasisi mbalimbali, hasa kuzingatia chama chake cha UDPS kimepata viti 66 vya wabunge sawa na asilimia 12 ya wabunge wote jambo ambalo kwa takwimu ni mafanikio.

Chama hicho kilipata viti 35 vya bunge kwenye uchaguzi wa mwaka wa 2018, mwaka huu kimepanda juu zaidi na kwa kujiongezea viti 31.

Muungano wa serikali unatokana vyama vinavyoongozwa na baadhi ya washirika wake muhimu wakiwamo Spika wa Seneti, Modeste Bahati Lukwebo, Waziri wa Ulinzi Jean Pierre Bemba na Waziri wa Uchumi, Vital Kamerhe.

Kutokana na matokeo hayo ni wazi Rais Tshisekedi ana wakati mgumu kuhakikisha washirika hao wanapata nafasi muhimu ndani ya serikali ili kujiimarisha kwenye uongozi wake.

Kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo, baada ya Mahakama ya Juu kuthibitisha matokeo ya uchaguzi, mshindi wa kiti cha urais ataapishwa Jumamosi wiki hii.

**MANUNG'UNIKO YAHANIKIZA**

Pamoja na kutangazwa kwa matokeo hayo, vyama vinavyomuunga mkono vimeanza kunung'unika kutokana na viti vyao kupungua na kunyooshea kidole chama cha Tshisekedi kwamba kimewapora kura.

Baadhi ya vyama vimemtilia shaka na kutoridhishwa na matokeo yaliyotangazwa na kueleza kwamba yamekuwa sawa na uteuzi wa wabunge, badala ya ushindani katika masanduku ya kura.

Hata hivyo, baadhi ya viongozi wamesikika wakisema wabunge wao wameshindwa kurudi bungeni kutokana na tabia ya kulipiziana kisasi ndani ya muungano huo.



Rais Felix Tshisekedi. **PICHA: MTANDAO**

> Wabunge zaidi ya 70 ambao ni watiifu wa Kabila wamepoteza nafasi zao baada ya kutogombea katika uchaguzi wa mwaka jana.



Moise Katumbi

**HASIRA ZAIBUKA**

Vyama vya upinzani na waangalizi huru wa uchaguzi wameelezea wasiwasi wao kuhusu kupatikana kwa wabunge hao kutokana na uchaguzi huo kutokuwa huru, haki na unaokubalika.

Tayari baadhi ya vyama vya upinzani vimetangaza kutotambua ushindi wa Tshisekedi na vyama washirika vikisema hawakuchaguliwa na raia wa DRC, bali walitokana na njia chafu na wizi wa kura.

Mshindi wa pili Moise Katumbi ameeleza uchaguzi uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Desemba 20, kuwa ni sawa na kichekesho kutokana na upigajikura kukumbwa na machafuko na kwenda kinyume na masharti ya upigaji kura.

Licha ya kelele za upinzani, Rais Tshisekedi anapata ahueni kutokana na serikali kadhaa za nchi za magharibi kumuunga mkono na mara alipotangazwa kuwa mshindi hazikusita kumpongeza.

Kwa upande wake Tume ya Uchaguzi ya DRC (CENI), imeendelea kujinasibu kuwa ulikuwa wa huru na uwazi ingawa ilibatilisha matokeo ya wagombea 82 wa nafasi za ubunge kati ya wagombea 100,000 waliowania nafasi hizo.

Mtihani mwingine ilioko mbele ya utawala wa Rais Tshisekedi ni ukosefu wa usalama mashariki mwa nchi hiyo hasa mashambulizi yanofanywa na waasi wa M23.

Katika kipindi chake cha kwanza ameshindwa kuwahakikishia wananchi wanaoishi mkoa ya Kivu Kaskazini usalama kutokana na kukabiliwa na mashambulizi na mauaji ya mara kwa mara yanayofanywa na vikundi vya waasi wanaotumia eneo hilo kama ngome zao kwa muda mrefu.

Katika hatua nyingine, Kanisa Katoliki ambalo linaaminiwa na Wakongo wengi limeeleza kuwa na mashaka na ushindi uliopatikana kwenye muungano huo, likisema uchaguzi ulikuwa na udanganyifu.

Rais Tshisekedi analazimika kufanya jitihada za kurudisha imani na kanisa hilo ambalo idadi kubwa ya wananchi wake ni waamini wake.

Awali ujumbe wa uangalizi wa Makanisa ya Kikatoliki na Kiprotestanti, ulionyesha kuwapo kwa udanganyifu katika kuhesabu kura na kugawa viti. Ujumbe huo ulikumbusha kwamba haiwezekani kuwahakikishia wadau wote uhalali wa kura wakati hauko tayari kukubali matokeo.

Katika matokeo hayo chama cha Moise Katumbi kilipata viti 20 pekee vya ubunge katika matokeo hayo, wakati rais wa zamani Joseph Kabila, ilisusia chaguzi huo, akiuelezea kuwa ulijaa vurugu na wizi wa kura kupita chaguzi zote zilizofanyika nchini humo.

"Tangu mwaka 2021, tulionya dhidi ya mchakato huu," anasema kada mmoja wa Chama cha PPRD, cha rais wa zamani, Joseph Kabila.

Anasema sababu za kutokuwa na imani na uchaguzi huo ni udhaifu wa taasisi, CENI na Mahakama ya Katiba, ambazo zinasimamia chaguzi hizo.

Wabunge zaidi ya 70 ambao ni watiifu wa Kabila wamepoteza nafasi zao baada ya kutogombea katika uchaguzi wa mwaka jana.

Mwaka 2018, Rais wa Congo wakati huo Joseph Kabila, alimchagua waziri wa zamani wa mambo ya ndani Emmanuel Ramazani Shadary, kuwa mrithi wake katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa lakini alishindwa na hata hivyo mwaka huu, hakusikika kwenye mchakato na kususia uchaguzi mkuu. **DW/ RFI**



## HABARI DODOMA

# TALGWU yawasilisha kero serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za MitaaTanzania (TALGWU), kimewasilisha kero kwa serikali ikiwamo ya watumishi wa afya kujilipia ada ya leseni ya kutoa huduma kila mwaka licha ya kuwaajiri.

Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha baraza kuu la chama hicho.

"Kuna manung'uniko makubwa kwa watumishi wa kada za afya kutakiwa kujilipia ada ya leseni kila mwaka huku wakitekeleza majukumu ya kutoa huduma kwa umma, na iwapo wanashindwa kulipia wanakosa haki ya kupandishwa daraja na vyeo, ikumbukwe hawafanyi biashara kwa leseni hizo," alisema.

Mtima alisema wanaiomba serikali kuhakikisha waajiri wanawalipia watumishi hao ada hizo kwa kuwa wanatumia leseni hizo kuwahudumia wananchi.

"Leseni ya kutoa huduma isiwe sehemu ya kigezo cha watumishi wa kada ya afya kupandishwa madaraja, pia kuna changamoto ya mfumo mpya wa upimaji utendaji kazi kwa watumishi wa umma," alisema.

Alisema serikali imetoa muda mfupi kwa watumishi wa umma kujisajili bila kuzingatia watumishi wengi wanafanya kazi kwenye mazingira ya pembezoni ambako kuna tatizo la mtandao.

Katibu huyo aliitaja kero nyingine ni kutotolewa elimu ya kutosha ya matumizi ya mfumo huo na kuomba serikali iongeze muda kujisajili.

Kadhalika, alisema kuna tatizo kwenye muundo wa utumishi katika upandishwaji vyeo na kubadilishwa miundo hasa kwa watumishi wasio walimu.

"Wanapotoka masomoni kujiendeleza muundo unawalazimu kupelekwa kwenye cheo cha chini cha kuanzia bila kuzingatia uzoefu katika utumishi wa umma tunaomba serikali ibadili utaratibu na kuzingatia uzoefu," alisema.

Akifungua kikao hicho, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi aliahidi serikali itaendelea kushughulikia kero hizo.

Katambi alisema serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na mazingira wanayofanyia kazi ili kuinua ufanisi.

Alisema serikali itaendelea kulinda na kuzingatia haki za wafanyakazi nchini na kuwataka waajiri kuhakikisha wanafuata matakwa ya sheria za kazi na kudumisha mahusiano mema kazini.

"Wanachama wote wa TALGWU mtambue kuwa ulinzi wa haki za wafanyakazi unaanzia kwa ninyi wenyewe kuzingatia dhana ya haki na wajibu, kama chama mnapaswa kuwakumbusha wafanyakazi kujiepusha na vitendo vinavyoenda kinyume na misingi na maadili ya utumishi wa umma," alisema.

## YPGEA yawapigia debe vijana

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI ya kiraia inayojishughulisha na masuala ya amani, maendeleo na uchumi kwa vijana nchini (YPDEA), imeiomba serikali kuwatengenezea mazingira mazuri ya ujasiriamali vijana ili wajiajiri na kujiepusha na vitendo viovu.

Mratibu wa Idara ya Vijana Taifa wa taasisi hiyo, Ashura Moshi alitoa ombi hilo kwenye kikao cha viongozi wa taasisi hiyo wenye nafasi za ngazi ya mkoa na wilaya kilichofanyika jijini hapa.

Alisema iwapo serikali itatengeneza mazingira mazuri, vijana wataungana na kupatiwa mikopo itakayowasaidia kujikwamua kiuchumi na kuondokana na tamaa ya kujihusisha na vitendo viovu ili kupata fedha za haraka.

Alitaja kero kubwa iliyopo kwa vijana ni kukosa mazingira mazuri na sahihi kuungana na kupatiwa mikopo.

Ofisa Kilimo YPDEA Taifa, Neema Chiboni, aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa vijana ili kuondokana na tabia ya kukaa vijiweni na kusubiri ajira wakati kuna fursa nyingi za kilimo, biashara na ufugaji.

"Serikali ikiwapa elimu ya ujasiriamali kilimo cha bustani biashara na ufugaji kwanza wataweza kujiunga kwa pamoja na kujiinua kiuchumi na wataondokana na kukaa vijiweni na kuilalamikia serikali kwa kutowatengenezea mazingira hayo," alisema.

Akifungua kikao hicho, Mshauri Mkuu wa Taasisi hiyo, Askofu Vicent Malenda alisema malengo yao ni kuwaunganisha vijana kwa ajili ya kuwapatia elimu ya ujasiriamali ili wajikomboe kiuchumi.




Vyombo vya moto vikipita kwa shida na kusababisha foleni kutokana na maji ya mvua yaliyotuama katika barabara ya Mtaa wa Lindi na Msimbazi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TIC yahamasisha Watanzania uwekezaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimewataka Watanzania kutumia mwaka 2024 kuongeza uwekezaji nchini.

Meneja Uhamasishaji Uwekezaji wa Ndani wa kituo hicho, Felix John alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea baadhi ya wawekezaji mkoani hapa ikiwa ni kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani.

John alisema ametoa rai hiyo kutokana na takwimu walizonazo kuonyesha kuwa kiwango cha uwekezaji kwa wazawa kimefikia asilimia 46.

Alisema maboresho yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kubadilisha sheria na kupunguza kiwango vya mtaji yamesaidia kuongeza idadi ya wawekezaji wanaosajiliwa na TIC baada ya kuanza kutekelezwa kwa sheria hiyo.

Alisema sheria hiyo mpya ya uwekezaji ya mwaka 2022 imepunguza thamani ya mtaji kwa mwekezaji wa ndani kutoka Dola za Kimarekani 100,000 hadi kufikia Dola 50,000 kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini kwa wazawa.

Alisema sheria hiyo namba 10 inatambua wawekezaji mahiri ambao hupata motisha kwa kupewa misamaha ya kodi ndani ya kipengele hicho cha mwekezaji mahiri.

John alisema kampeni ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani inalenga kubadilisha fikra kwa Watanzania kuwa uwekezaji unawalenga wageni au wazungu tu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema TIC kuanzisha kituo cha utoaji huduma mahali pamoja ni hatua nzuri katika kumsaidia mwekezaji kupata huduma kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kupunguza usumbufu.

Kaimu Karibu Tawala Msaidizi Viwanda na Biashara Mkoa wa Singida, Lucas Mkuki, aliwakaribisha wawekezaji mkoani hapa kwa kuwa jiografia inafanya uwe kivutio kikubwa kutoka na kuwa na miundombinu mizuri ya barabara na maeneo ya kilimo.



# Mgambo wadaiwa kumwagia maji vitanda wasiolipa kodi

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

WANANCHI wa Kijiji cha Wangutwa Kata ya Uhambule Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe wamelalamikia kukithiri kwa michango inayodaiwa kutozwa na uongozi wa serikali ya kijiji ambayo imekuwa kero kwao.

Walitoa malalamiko hayo kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Njombe ikiwa imeongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ambao walifika kijijini hapo kwa lengo la kusikiliza kero mbalimbali kupitia mkutano wa hadhara.

Wananchi hao walisema wanapokubaliana aina ya michango katika mikutano ya kijiji viongozi wamekuwa wakiongeza kiasi cha fedha ambacho wamekubaliana au kuweka michango bila ya mpangilio.

Walisema wakati mwingine mgambo wanapita nyumba kwa nyumba kudai michango, endapo mhusika asipokuwa na fedha anapigwa kisha mgambo hao huingia ndani na kumwagia maji kitanda.

Kwa upande wake, Jafari Mnenwa alisema hapo awali walikubaliana kuchanga michango kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kabla hawajakamilisha hilo viongozi wakaja na michango mingine. "Tunampango wa kujenga madarasa, kabla hatujamaliza kujenga tunachangishwa fedha kwa ajili ya kununua kiwanja kwa ajili ya kujenga ofisi ya kijiji," alisema Mnenwa.

Mnenwa alisema katika mikutano yao walikubaliana kwamba atakayechelewa kutoa mchango atamlipa mgambo Sh.5,000 lakini jambo la kushangaza mgambo hao hudai Sh.10,000.

Mnenwa alisema amekuwa akifuatialia changamoto kijijini hapo na kuhoji lakini matokeo yake ameishia kusingiziwa kesi kwamba ameiba sola ambayo alinunua Sh.160,000.

Elida Ndalagwa alisema: "Mimi ni mjane mashamba yangu yamevamiwa na ndugu wa mume wangu, ambao wanalima pale lakini wakaenda polisi kunishtaki kwamba nimewatishia na panga, hivyo nikakamatwa nikapelekwa Kituo cha Polisi Ilembula nikalala mahabusu kulikuwa na askari polisi wawili wa kike na wa kiume wakanichukulia hela zangu Sh.150,000," alisema.

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Wangutwa, Ester Mrunwa alisema hayo ni makubaliano kupitia mkutano wa hadhara ambapo mchango walikubaliana kuwa Sh. 5,000 kwa ajili ya kununua kiwanja na walipeana muda kwamba ambaye atachelewa atakamatwa na atalipa gharama za mgambo Sh. 10,000, kauli ambayo imepingwa na wananchi hao. Kufuatia malalamiko hayo Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Wanging'ombe, Magnus Milinga alisema walipata taarifa kwamba Jasari (Jafari Mnenwa) anazo mali za wizi na anachochea uvunjifu wa amani.

"Baada ya kupata hivyo taarifa tulikuja kupekua na baadhi ya mali na ambazo tulijua ni mali yake halali tulimkabidhi, tulimkuta na sola pamoja na pikipiki ya wizi," alisema Milinga.

Akijibu tuhuma zinazomkabili Jafari Mnenwa alimueleza Mkuu wa Mkoa kwamba tangu ameanza juhudi zake za kufichua matukio ikiwemo ya wizi kijijini hapo amekuwa akipokea vitisho vingi ikiwemo kuitwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

"Tangu nimeanza kufuatilia changamoto za kijiji hiki ikiwemo wizi wa ng'ombe ambao mimi kwa kushirikiana na wenzangu tulizikamata kijiji cha jirani na mwenyekiti akiwa amefoji nyaraka ya mauziano, lakini polisi walikuja pale kwangu kufanya upekuzi eti mimi mwizi mbona haikuwa hivyo kipindi cha nyuma na iwe sasa au kwa sababu nimejitolea kufuatilia mambo," alisema Mnenwa.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alipiga marufuku kuwepo michango kwa sasa hadi pale wananchi hao watapokubaliana upya.

Mtaka alisema: "Mh. Diwani naomba hii michango isimame hawa watu walime, wafanye shughuli za mavuno na wakivuna mtakaa sasa mkubaliane shughuli za kimaendelea mnafanyaje".



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (kushoto), akishirikiana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga, kukata utepe jana, kuzindua magari yaliyonunuliwa na serikali kwa ajili ya jeshi hilo, kukabiliana na uhalifu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Polisi watakiwa kutotumia nguvu kukabiliana na uhalifu

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeshauriwa kutotumia nguvu wakati wa kukabiliana na uhalifu, badala yake litoe elimu kwa wananchi ili waweze kusaidia shughuli za kuzuia uhalifu.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa wakati akikabidhi magari matatu yaliyonunuliwa na serikali kwa ajili ya Jeshi la Polisi kukabiliana na uhalifu.

Alisema kuwa suala la usalama wa raia na mali zao siyo la polisi pekee bali la kila mwananchi, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa wananchi kushirikishwa katika suala la kukabiliana na uhalifu.

"Tunahitaji kuifanya jamii yetu iishi kwa amani na utulivu, lakini ili tufanikiwe hatuwezi ni lazima wananchi washirikishwe kwa kupewa elimu ya kukabiliana na uhalifu, polisi msitumie nguvu pekee kukabiliana na uhalifu bali waelimisheni wananchi ndipo tutafanikiwa," alisema Malisa.

Alisema kuwa utaratibu wa sasa wa Jeshi la Polisi kupeleka askari katika kila kata ni mzuri kwa kuwa askari hao wakichangamana na jamii wanaweza kuzuia uhalifu kabla haujatokea na kuifanya jamii iishi kwa amani na utulivu.

Akipokea magari hayo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga alisema magari hayo yatalisaidia Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa weledi wakati wa kukabiliana na wahalifu.

Alisema kupatikana kwa magari hayo kutaongeza vitendea kazi kwa askari wa jeshi hilo ambao watayatumia kufika maeneo mbalimbali kwa wakati kwa ajili ya kudhibiti uhalifu.

"Magari haya yatatusaidia kufika kila mahali kukabiliana na uhalifu, lakini pia yatatufanya tuwahi kwenye maeneo yenye viashiria vya kutokea uhalifu na kuvidhibiti kabla uhalifu haujatokea na kuathiri wananchi," alisema Kuzaga.

Alisema kutoka na kasi ya uboreshaji wa vitendea kazi vya Jeshi la Polisi unaofanywa na serikali, anaamini kuwa utafika wakati ambao wilaya zote za Mkoa wa Mbeya zitakuwa na magari mapya ambayo yatatumika kudhibiti uhalifu kwa wakati mpaka maeneo ya vijijini.

Kamanda Kuzaga alisema kwa mwaka huu Jeshi la Polisi mkoani Mbeya limejipanga kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili washirikiane katika kudhibiti uhalifu na wahalifu kwa lengo la kuifanya jamii iishi kwa amani na utulivu.

# RC apendekeza kufutwa ada vyuo vya maendeleo ya jamii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ameiomba serikali kufuta ada katika vyuo vya maendeleo ya jamii kama ilivyo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini ili kuwezesha vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo ya sekondari kujiunga na vyuo hivyo.

Homera alitoa ombi hilo juzi mbele ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilipofanya ziara mkoani Mbeya kwa lengo la kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya TAMISEMI.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya elimu Mkoani Mbeya, Homera alisema kuwa wameazimia kuwapeleka vijana wanaohitimu darasa la saba na kushindwa kuendelea na elimu ya sekondari katika vyuo ya maendeleo ya jamii ili wajiendeleze kielimu.

Alisema uamuzi huo ulifikiwa na serikali ya mkoa baada ya kubaini kuwa wanafunzi wanahitimu darasa la saba wakiwa na umri mdogo na wanapofeli mtihani wa darasa la saba na kutochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari huingia mitaani bila kuwa na uwezo wa kujitegemea.

"Kwa kuwa watoto hawa wanakuwa na umri mdogo ambao hawawezi kujitegemea, wasipochaguliwa kwenda sekondari wanaingia mitaani na kujihusisha na vitendo vya uhalifu wa kuvuta bangi au kujiita panya road ambao wanaanza kuvamia watu na kuhatarisha amani na utulivu kwenye jamii," alisema Homera.

Alisema ili kuwaepusha vijana hao kujiingiza kwenye uhalifu, mkoa uliamua kuwapeleka kwenye vyuo vya maendeleo ya jamii ambako wanafundishwa ujuzi wa aina mbalimbali kama vile ufundi cherehani, uashi, uselemala au mapishi, ujuzi ambao baadaye unawasaidia kufanya shughuli za kujitegemea.

Alisema hata hivyo wanafunzi hao wanapofika vyuoni wanatakiwa kulipa ada isiyopungua shilingi 250,000 hali ambayo baadhi yao hushindwa kulipa na kurejea mitaani.

"Ikiwa taifa hili linahitaji kutokeza panya road, naiomba Kamati hii ya Bunge iniunge mkono na kufikisha ombi hili serikali kuomba ada katika vyuo hivi ifutwe ili tuwasaidie vijana wetu," alisema Homera.

Alisema kuwa hatua ya kufuta ada kwenye vyuo hivyo pia itajenga usawa miongoni mwa watoto wanaokwenda kusoma sekondari ambao wamefutiwa ada mpaka kidato cha sita huku watoto wenye sifa kama hao wakitozwa ada kwenye vyuo vya maendelo ya jamii.

Akizungumzia ombi hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa, Dennis Londo alisema wamelipokea na wanaunga mkono hoja hiyo.

## Wakala wa vipimo kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) wametiliana saini hati ya makubaliano ya ushirikiano ili kuimarisha utendaji kazi.

Akizungumza juzi baada ya kushuhudia utiaji saini huo uliofanyika visiwani hapa, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara (SMT), Dk Hashil Abdallah alisema ni vyema kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo ili kuhakikisha vipimo vyote na thamani ya fedha inamfikia mtumiaji kwa usahihi.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya vipimo, wakala hao ndio taasisi pekee inayopaswa kusimamia matumizi sahihi ya vipimo vinavyotumika katika biashara ili kuepusha madhara yatokanayo na vipimo batili na kulinda walaji na watumiaji.

Alisema makubaliano hayo yatasaidia kuimarisha utendaji wa kazi, kuongeza ufanisi na kufikia malengo ya taasisi hizo.

Mkurugenzi wa Wakala wa Vipimo Zanzibar, Hammed Simai Mwalim alisema iwapo vipimo vitasimamiwa kwa usahihi bidhaa Serikali itakusanya kodi sahihi kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Aliwataka wananchi na wafanyabiashara nchini kuhakikisha wanatumia vipimo sahihi na endapo watakutana na changamoto wafike kwenye ofisi za wakala hao kupata msaada wa kitaalamu.

Aliwaonya baadhi ya wafanyabiashara kuacha mtindo wa kuchezea vipimo kwa lengo la kuwaibia wananchi kwani ni kosa kisheria na hatua kali zitachukuliwa kwa watakaobainika.

**Alisema makubaliano hayo yatasaidia kuimarisha utendaji wa kazi, kuongeza ufanisi na kufikia malengo ya taasisi hizo.**

# NCCR yawachimba mkwara wanachama kuandamana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha NCCR Mageuzi kimewataka wanachama wake kutoshiriki maandamano yaliyopangwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kufanyika nchini Januari 24, mwaka huu na kuonya kuwa watakaokiuka watachukuliwa hatua kali.

Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi, Haji Ambar Khamis alitoa kauli hiyo jana visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandamano hayo.

Khamis alisema kuwa chama hicho kimezuia wanachama wake kushiriki maandamano hayo baada ya kubaini kuwa siyo suluhisho na kuonya kuwa atakayeshiriki adhabu kali itachukuliwa dhidi yake.

Alisema chama hicho hakijaona sababu ya msingi ya kushiriki katika maandamano hayo kwa sababu madai yanayoenda kuungwa na CHADEMA katika maandamano hayo kuhusu miswada ya sheria, siasa na uchaguzi iliyowasilishwa Bungeni NCCR imetoa maoni yao na kuyawasilisha kwenye muhimili huo.

"Maoni yetu tuliyowasilisha Bungeni bado hatujapata mrejesho, tusubiri kwanza majibu yatakayotoka Bungeni kama hayajaturidhisha ndio tutaamua cha kufanya," alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema maoni yao waliyowasilisha Bungeni kuhusu miswada ya sheria yanayohusu masuala ya siasa na uchaguzi baadhi wanaunga mkono kwa maslahi ya nchi na yapo ambayo waliyapinga kwa sababu yamepitwa na wakati.

"Kuna kawaida wapo watakaojifanya ni wanachama wa NCCR Mageuzi kushiriki katika maandamano hayo, lakini tunatoa indhari ya kwamba hao sio wanachama wetu wamejivisha tu joho ili waonekane wanachama na lolote litakalowafika chama hakitahusika," alisema.

Alisema NCCR imewasilisha barua kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania (IGP) kusimamisha mikutano ya kisiasa nchi nzima kwa chama hicho baada ya kubaini kuwa baadhi ya waliojitokeza kuomba kufanya maandamano na mkutano wa hadhara bila ya ridhaa ya chama hawakuwa wanachama halali.

"IGP tunamwambia mtu yeyote atakayejifanya kuwa ni mwanachama wa NCCR Mageuzi akashiriki maandamano hayo amchukulie hatua. NCCR kwa mapana na marefu tunasema hatutakuwa miongoni mwa watakaoshiriki katika maandamano hayo yaliyoandaliwa na CHADEMA," alisisitiza.

Hata hivyo alisema, chama hicho kinajiandaa kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa, licha ya kukabiliwa na migogoro baina yao na aliyekuwa mwenyekiti wake, James Mbatia.

Mwenyekiti huyo alisema NCCR imeipongeza Serikali ya Zanzibar wa kusherehekea miaka 60 ya mapinduzi kwa amani na utulivu.




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kushoto) na Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Balozi Téte António wakionyesha hati za makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi na kuondoleana visa/pasi kwa wenye hati za kusafiria za kidiplomasia na za kikazi, baada ya kutiliana saini mjini Zanzibar jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# SMZ yazibana mamlaka utoaji leseni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imezitaka mamlaka zinazohusika na utoaji leseni kufuata sheria na miongozo ili kuboresha huduma kwa wananchi na kuondoa urasimu.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban aliyasema hayo juzi wakati wa Maadhimisho ya Siku ya leseni na miaka 10 ya kuanzishwa Baraza la Usimamizi wa Utoaji wa Leseni.

Shaaban alisema kuna mamlaka hazifanyi kazi vizuri, hivyo watakapofuata sheria na miongozo itasaidia upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

Alisema ni lazima mamlaka hizo ziwe na mkataba wa huduma kwa wateja ili mtu anapokwenda kuomba leseni kuwa na uhakika wa kuipata ndani ya saa 24.

Waziri Shaaban alisema baraza hilo linatakiwa kuhakikisha dhana ya leseni inatumika kama huduma na siyo chanzo cha mapato ili kurahisisha uzalishaji wa biashara.

Alisema kuna mamlaka za leseni ambazo ni chanzo kikuu cha mapato na kuongeza malipo katika leseni, vibali vya ruhusa kila mwaka, jambo hilo halikubaliki kwa mujibu wa sheria ya udhibiti wa mifumo ya leseni.

Alisema bado Zanzibar mfumo wa utoaji huduma haufanyi vizuri hivyo baraza hilo kwa kushirikiana na wakuu na taasisi hizo linatakiwa kuhakikisha linapata sifa stahiki.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis Juma alisema taasisi hiyo ina umuhimu mkubwa katika utendaji kazi na kuwadhibiti watoaji leseni.

Alisema wizara yake kupitia taasisi hiyo inafanya kazi ya kuondoa malalamiko ya kuwepo kwa utitiri wa leseni, vibali na tozo.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Hawa Ibrahim Mbaye alisema lengo lao ni kuleta mafanikio na kuondoa urasimu katika utendaji kazi.

Alisema baraza hilo litaendelea kusimamia, kusisitiza, kuongeza mikakati na kufuata miongozo ya biashara ili kupunguza urasimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUDI JOSEPH WILLIAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3609/0034** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IGALULA SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/6137/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SCOLA MUSA SEME** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba S.2282/0027 kilichotolewa na Baraza la Mitihani ya Taifa kupitia **IKINGA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Kwa yeyote atakayekiona atoe kituo chochote cha Polisi.
**TAARIFA ya Polisi PHQ/MBE/MBE/814/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MARIAM MWINYIHAMISI MUSHI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 285576** iliyotolewa na makao makuu **PCO, DAR ES SALAAM mwaka 2020.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PRINCE NAFTARI BONIMATO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3533/0180** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI KAWE UKWAMANI** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/5108/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 01 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANNA JOSEPH TARIMO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY ALBERT PASCAL CHAKI & PASCAL CYRIL CHAKI**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of the Probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made on the above –named petitioner.
The petition has been fixed for Mention on 22nd Day of Jan 2024 before Hon.Ruth Mkisi –SRM
Objections to the grant should be filed on or before the 22nd day of jan 20204
Dated at Moshi this 03 day of jan 2024

**Senior Resident Magistrate**
**MOSHI**

## TANGAZO LA MNADA

Work ethic Auctioneer Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari Jijini Dar es salaam na Moshi Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| JOSEPHAT BITTA MAGESA | TOYOTA HARRIER T189 ECN | 31.01.2024 |
| JAMES JAMES CATHBELT | SUBARU RI T452 EAE | 31.01.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga**
**0677014355(Fanikiwa)**
**0713197485(Work Ethic)**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YASINI HAMISI NDALIMO**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 437 DJK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/LIN/LIN/1545/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**NGABANYA GILU NYASUBI**

mjini Kahama anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T.993 CKA** na **T.986 CKA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake, Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/28/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KKKT DAYOSISI YA KASKAZINI FUKENI MBOKOMU LUTHERAN PARISH**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 377 AKD** Toyota Hilux .Chassis namba **LN1060117396,** Engine namba **3L3864747** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taafifa : **PHQ/KIL/MOS /5970/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**

**WILAYA YA MOROGORO, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...61/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: BEISON MARTIN RAPHAEL wa MTONI STREET-MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ALEX MWEKA MUHOCHI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 24 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 01 mwaka 2024

..........................................
**HAKIMU**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa Tupigie 0745 700 710.***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Rais Weah: Sitagombea tena urais

**MONROVIA,** Liberia

RAIS anayemaliza muda wake wa Liberia George Weah (pichani) amesema hana mpango wa kutaka kuchaguliwa tena mwaka 2029 baada ya kushindwa katika uchaguzi wa hivi karibuni.

Inaelezwa kuwa kiongozi huyo alichaguliwa mwaka 2017 lakini alishindwa katika uchaguzi wa Novemba 2023 na mpizani wake Joseph Boakai. Huku akisema atakuwa na umri wa miaka 63 baada ya miaka sita, na hatakuwa tayari kujihusisha na siasa zaidi akiwa na miaka hiyo.



"Nina miaka 57 sasa na umri wetu wa kustaafu ni miaka 65 na miaka sita kuanzia sasa nitakuwa 63 na siwezi kufanya kazi kwa miaka miwili, pia ninahitaji wakati kwa ajili yangu, watoto na familia," alisema na kuongeza;

"Sikuja kwenye siasa ili kuchukua mamlaka, hamtanivuta kwenye siasa hadi nifikishe miaka 90, nasema asanteni Waliberia kwamba nimekuwa rais iwe mara moja au mara 50, lakini ninaweza kuwahakikishia kuwa ni mara moja," alisema Weah.

Aidha, ilielezwa kuwa hakubainisha alichopanga kufanya baadaye, licha ya kuhimiza amani na ustawi katika nchi yake.

Hata hivyo katika hotuba yake iliyosifiwa na watu wengi mwezi Novemba, 2023 Weah, alisema chama chake cha 'Congress for Democratic Change' (CDC) kitasalia kuwa upinzani mkali katika taifa hilo. **BBC**

# Suala la majaji laibua sura mpya Kenya

**NAIROBI,** Kenya

JAJI Mkuu wa Kenya, Martha Koome amesema idara ya mahakama imemwandikia barua Rais William Ruto kutaka kushughulikia maswala aliyoibua kuhusu baadhi ya majaji.

Kauli hiyo imekuja baada ya siku chahe zilizopita Rais Ruto kuwashutumu baadhi ya majaji ambao hawakutajwa kuwa wanafanya ufisadi kwa kushirikiana na upinzani katika kuzuia miradi ya serikali yake.

**Ilielezwa kuwa kodi mbili mpya za ushuru wa nyumba na makato ya bima ya afya kwa wote zimepingwa kortini.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana Jaji Koome, alisema mashambulizi dhidi ya mahakama yanatishia kuifanya nchi kuwa na machafuko.

"Iwapo mwelekeo huu utaachwa kuendelea bila kusitishwa, tuko kwenye ukingo wa mgogoro wa kikatiba ambao unaweza kusababisha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Kwa hivyo tutalenga kufanya mazungumzo hayo, tumeandika barua na ninaamini kuwa rais atatupa muda," alisema Jaji Koome.

Aidha, kutokana na suala hilo inaelezwa kuwa kiongozi wa upinzani, Raila Odinga alimkashifu Rais Ruto kwa kujaribu kuwatisha majaji huku kundi la mawakili likifanya maandamano wiki iliyopita kwa lengo la kulaani mashambulizi ya kiongozi wa taifa hilo.

Hata hivyo tangu Kiongozi hiyo aingie madarakani Septemba 2022, amekuwa akikosolewa kwa madai ya kuanzisha ushuru mpya katika bidhaa za biashara, huku Wakenya wakitajwa kulalamika kutukana na kupanda kwa gharama za maisha.

Vile vile ilielezwa kuwa kodi mbili mpya za ushuru wa nyumba na makato ya bima ya afya kwa wote zimepingwa mahakamani, na maamuzi yake bado yanasubiriwa. **BBC**



Donald Trump akiwashukuru wapigakura wa Iowa kwa kumpa ushindi kwenye kura za mchujo, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Republican wamchagua Trump kuwania urais

**WASHINGTON,** Marekani

ALIYEKUWA Rais wa Marekani Donald Trump ameshinda kwenye kinyang'anyiro cha kwanza cha kuwania uteuzi wa kugombea urais wa taifa hilo kupitia Republican akithibitisha jinsi alivyo na nguvu licha ya kukabiliwa na msururu wa kesi mahakamani.

Akiwahutubia wapigakura wa chama chake kwenye uchaguzi huo uliofanyika jana katika jimbo la Iowa, alisema hilo ni tukio la fahari kubwa kwao akieleza kuwa hiyo ni mara ya tatu kwa wao kushinda.

"Lakini huu ni ushindi mkubwa kabisa, walisema ukishinda kwa asilimia 12 ni ushindi mkubwa, hilo litakuwa jambo gumu kulifikia, lakini nadhani tumepindukia mara mbili, nakisia hata pengine imepindukia mara tatu," alisema Trump.

Ilielezwa kuwa bilionea huyo mwenye umri wa miaka 77 alipata asilimia 51 ya kura, akifuatiwa na Gavana wa Florida, Ron DeSantis, aliyepata asilimia 21 na balozi wa zamani wa Marekani kwenye Umoja wa Mataifa, Nikki Haley, aliyepata asilimia 19.

Huo unatajwa kuwa ushindi mkubwa zaidi kuwahi kupatikana kwa mtia nia ya kuwania urais kupitia Republican, tangu ule wa Bob Dole aliyeshinda kwa tofauti ya asilimia 12.8 mwaka 1988.

Inabainishwa kuwa ushindi wa Trump kwenye jimbo hilo unaonyesha kutokuyumba kwa wafuasi wake hata baada ya uvamizi wa Januari 6, 2021 dhidi ya jengo la bunge, na mashitaka 91 ya uhalifu dhidi yake kwa kujaribu kuyapindua matokeo ya uchaguzi wa 2020.

Mashitaka mengine anayotuhumiwa nayo Trump ni kukutwa na nyaraka za siri baada ya kuondoka madarakani na kughushi taarifa za malipo ya fedha kwa muigizaji mmoja wa sinema za uchafu.

Aidha, ilielezwa kuwa Trump ametumia matatizo yake hayo ya kisheria kuchangisha fedha na kuongeza ufuasi wake, akijenga hoja kwamba yeye hana makosa bali amefanywa tu kuwa mbuzi wa kafara katika mchezo wa kumsaka mchawi.

Hata hivyo ilibainishwa kwamba uchunguzi wa maoni unaonyesha kuwa zaidi ya nusu ya wapigakura wa Republican wanayaamini madai ya Trump kwamba ushindi wake kwenye uchaguzi wa mwaka 2020 uliibiwa, wakisema hawadhani kwamba ni kweli Rais wa Marekani Joe Biden alimshinda kihalali Trump.

Zaidi ya asilimia 60 wanasema kuwa bado Trump anafaa kuwa rais hata kama atatiwa hatiani kwa uhalifu anaoshitakiwa nao.

Kihistoria, jimbo la Iowa limekuwa likichukuliwa kama kigezo cha mwenendo wa uchaguzi kutokana na kuwa la awali kwenye kalenda ya kampeni, licha ya kwamba si kila mara mshindi wa jimbo hilo humaliza kwa kuwa mgombea urais, kama ilivyotokea mwaka 2008, 2012 na 2016.

Hata hivyo inaelezwa kuwa Trump anataka kuuharakisha mchakato huo, ambao kwa kawaida unachukuwa miezi kadhaa, kwa kuhakikisha kuwa anapata ushindi mkubwa kwenye chaguzi za awali ili kuwalazimisha washindani wake kujiondoa mapema.

Ilibainishwa kuwa wa kwanza kufanya hivyo alikuwa Vivek Ramaswamy, ambaye baada ya kupata asilimia nane tu ya kura hapo jana, alitangaza kujitowa kwenye kinyang'anyiro hicho na badala yake akawataka wafuasi wake kumuunga mkono Trump. **DW**

# JENTRIX SABABU JOELLE KUTOLEWA KWA MKOPO

**Saada Akida na Oliver Albert**

VITA kubwa ya namba ndani ya kikosi cha Simba Queens ikiwa ni pamoja na kurejea kwa straika Jentrix Shikangwa ndani ya timu hiyo kumemfanya kiungo mshambuliaji, Joelle Bukuru kutolewa kwa mkopo kwenda Klabu ya Fountain Gate Princess hadi mwishoni mwa msimu huu.

Hata kabla ya kurejea kwa Jentrix kutoka Beijing, Jingtan ya China, Joelle raia wa Burundi alikuwa katika vita kubwa ya namba na mapro wenzake akiwamo Mkenya Vivian Corazone, Mzimbabwe Danai Bhobo na Mganda Riticia Nabboss aliyesajiliwa msimu huu.

**Jentrix aliwahi kuwa mshambuliaji wa timu hiyo na msimu uliopita alimaliza akiwa mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini kwa kupachika mabao 25, kabla ya kupata dili hilo la kujiunga na Beijing Jingtan ya China, alipodumu kwa miezi sita.**

Vivian amejihakikishia namba kikosini na ni mmoja wa nyota wanaoibeba Simba Queens kwenye michuano mbalimbali wakati Danai na Riticia nao tayari wameshaingia kwenye mfumo wa makocha wa timu hiyo na wamekuwa wakianza kikosi cha kwanza katika mechi nyingi za hivi karibuni.

Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, aliwaambia waandishi wetu kuwa ushindani wa namba ndani ya kikosi hicho umesababisha kufanya uamuzi wa kumtoa kwa mkopo Joelle ili akalinde kiwango chake.

"Joelle ni mmoja wa wachezaji bora katika kikosi chetu, lakini kwa sasa ushindani wa namba ni mkubwa unaosababisha kushindwa kupata nafasi na ndio maana klabu imeamua kumpeleka kwa mkopo Fountain Gate.

"Kama uongozi na benchi la ufundi lina imani kubwa na Joelle na tunaamini atafanya vizuri katika timu yake mpya na baada ya mkopo wake kumalizika anaweza kurudi Simba," alisema Makanya.

Joelle alijiunga na Simba Queens mwaka 2018 na ameichezea timu hiyo kwa misimu mitano na amekuwa kipenzi cha mashabiki wa klabu hiyo kutokana na urembo wake.

Hata hivyo, kwa mujibu wa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, kimeeleza "kulikuwa na timu nchini Uturuki inataka huduma ya Joelle, lakini ofa hiyo imekufa wakati tayari viongozi wamemrejesha Jentrix kuja kuchukua nafasi ya kiungo".

## Dar City kuongeza watatu tu

**Na Oliver Albert**

MABINGWA wa Ligi ya mpira wa Kikapu Mkoa wa Dar es Salaam (RBA), Dar City, wamepanga kuongeza wachezaji wasiozidi wanne kwa ajili ya msimu mpya wa ligi hiyo mwaka huu.

Dar City ambayo ilishiriki RBA kwa mara ya kwanza mwaka jana na kutwaa ubingwa, imepanga kuendeleza moto wao kwenye ligi ambayo inatarajiwa kuanza baadaye Mei, mwaka huu.

Timu hiyo iliweka rekodi kwenye RBA kwa kucheza michezo 13 bila kupoteza huku mchezo mmoja ukishindwa kufanyika baada ya kufanana rangi ya jezi na ABC, hivyo wapinzani wao hao kupewa ushindi wa mezani.

Kocha wa Dar City, Mohammed Mbwana, alisema kwa jinsi anavyoona kikosi chake, hana haja ya kusajili wachezaji wengi kwani anaamini waliopo wanaweza kufanya maajabu.

"Ili jambo lako liwe zuri, lazima kila baada ya muda uweze kufanya maboresho kwenye timu, lakini nikiangalia kwa kikosi nilichokuwa nacho mwaka jana bado ni bora na kinaweza kushiriki kwenye ligi na kikafanya vizuri.

"Ili kuleta chachu zaidi kuna sehemu tutaongeza wachezaji kama watatu tu katika nafasi ya katikati (Centre), mshambuliaji (Power Forward) na mchezeshaji (Point Guard)," alisema Mbwana.

Pia Mbwana alisema hawakufanya vizuri kwenye Mashindano ya Klabu Bingwa (NBL), msimu uliopita kutokana na maandalizi duni waliyofanya.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibasila, Shuagod Julius (kushoto) na Hassan Karim, wakicheza mpira wa kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Omary kinara gofu mil. 60/- zikikusanywa

**Na Oliver Albert**

ABBE Omary ameibuka mshindi wa jumla baada ya kupiga mikwaju ya neti 72 katika mashindano maalumu ya gofu ya Lions Club, Dar es Salaam Mzizima, yakiwa ni maalumu kwa kuchangia fedha kwa ajili ya huduma za macho.

Katika mashindano hayo yaliyoshirikisha wachezaji 50 kutoka Klabu za Dar es Salaam Gymkaha, Lugalo na Kilombero huku wakitumia viwanja 18, Omary alifuatiwa na Son Vengetsamy aliyepiga mikwaju ya neti 73 huku kwa upande wa daraja A nafasi ya kwanza ikichukuliwa na Shabir Abji aliyeshinda baada ya kupiga mikwaju ya neti 74 akifuatiwa na Taha Jabiri aliyepata neti 79 wakati daraja B mshindi akiwa ni Kanal Lkhani aliyepiga mikwaju ya neti 74, akifuatiwa na George Parira aliyepata neti 77.

Mratibu wa Kambi za Macho za Lions Club Mzizima, Ragib Hassanali, alisema jumla ya Sh. milioni 60 zilikusanywa katika mashindano hayo yaliyofanyika Jumamosi kwenye Uwanja wa Gymkhana jijini Dar es Salaam.

## Zimamoto kamili mbio za ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAAFANDE wa Klabu ya Zimamoto wamesema kuelekea mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, timu hiyo imejipanga kuhakikisha inaanza kwa kishindo kikubwa mzunguko wa lala salama.

Zimamoto SC ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 30 ambapo imeshinda michezo tisa, imefungwa mitatu na sare tatu katika mechi 15 ilizocheza za mzunguko wa kwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo Mohmed Suleiman 'Tangisho' alisema katika kuhakikisha wanafanikiwa mipango yao hiyo timu hiyo imefanya usajili mzuri wa kukiimarisha kikosi chake hicho.

Alisema usajili walio ufanya umeenda sambamba na matakwa ya benchi la ufundi la timu hiyo kutokana na tathmini yao waliyoifanya katika michezo ya mzunguko wa kwanza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS BASI TENA

NEWCASTLE United imesitisha harakati zao za kumnunua kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, 28, kwa sababu ya takwa la Manchester City la kutaka ada ya mkopo. ***(Telegraph)***

### PALACE, EVERTON ZAMTAKA

KLABU za Crystal Palace, Everton, West Ham na Juventus pia zina nia ya kumsajili Kalvin Phillips. ***(Sky Sports)***

### BENZEMA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA pia wanafuatilia Ligi ya Saudia na wanaweza kumnunua mshambuliaji wa Al-Ittihad na Ufaransa, Karim Benzema, 36 au fowadi wa Brazil, Roberto Firmino (32), ambaye alijiunga na Al-Ahli msimu wa majira ya joto. ***(Goal)***

### BRUNO AWINDWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes,26, ambaye ana kipengele cha kuachiwa cha pauni milioni 100. ***(Talksport)***

### STRAIKA ATAFUTWA UNITED

BILIONEA Sir Jim Ratcliffe anataka kumsajili mshambuliaji wa kati wa daraja la juu, ambaye yuko katika kiwango sawa na mshambuliaji wa Bayern Munich, Harry Kane, 30, mara tu mkataba wake wa kununua hisa asilimia 25 ya Manchester United utakapoidhinishwa na Ligi Kuu. ***(Standard)***

### OLISE ANUKIA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imejadili uwezekano wa kumnunua winga wa England, Michael Olise, 22, msimu wa majira ya joto na watakuwa tayari kumruhusu mlinzi wa England, Aaron Wan-Bissaka, 26, kuhamia Crystal Palace. ***(ESPN)***

### ARAUJO LULU SOKONI

MANCHESTER United pia wameungana na Bayern Munich katika harakati za kumsajili beki wa Barcelona, kutoka Uruguay, Ronald Araujo, 23. ***(Florian Plettenberg)***

### SANCHEZ SASA KUHAMA

KIUNGO wa kati wa Ureno, Renato Sanches huenda akahama mwezi huu kwani Paris St-Germain hawamtaki beki huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye anacheza kwa mkopo Roma ambao nako omeambiwa atafute klabu nyingine. ***(Fabrizio Romano)***

### LINGARD KUSEPA MAREKANI

MCHEZAJI huru, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 31, yuko tayari kuhamia Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS. ***(Mail)***

### DURAN MKATABA MFUPI

KLABU ya Chelsea inaweza kuvutiwa na mkataba wa mkopo wa muda mfupi kwa mshambuliaji wa Aston Villa, Colombia Jhon Duran, 20. ***(Nathan Gissing, kupitia Metro)***

## DOND… SOKA MAGAZ… LAYA



# MESSI ATWAA TUZO FIFA

## ●●● Awabwaga Haaland, Mbappe, huku Guardiola naye akibeba...

**LONDON,** England

LIONEL Messi ameshinda tuzo yake ya tatu ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), ya mwanasoka bora wa mwaka 2023, akiwashinda Erling Haaland wa Manchester City na mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe kwenye kinyang'anyiro hicho.

**Muda wa tuzo hiyo ulikuwa kati ya Desemba 19, 2022 - siku moja baada ya Messi kuiongoza Argentina kushinda Kombe la Dunia nchini Qatar - na Agosti 20, 2023.**

Messi alishinda tuzo hiyo zaidi kwa kazi yake ya PSG na Inter Miami, baada ya kuwasaidia wababe hao wa Ufaransa kutwaa taji lingine la Ligue 1 kabla ya kuhamia MLS Julai na kuiwezesha Miami kutwaa taji lao la kwanza kabisa, Kombe la Ligi.

Katika kiwango cha kimataifa, Messi aliisaidia Argentina kuongoza jedwali la kufuzu kwa Kombe la Dunia la Fifa la 2026 kupitia CONMEBOL (Shirikisho la Soka la Amerika Kusini), baada ya michezo sita.

Messi hakuhudhuria London kuchukua tuzo hiyo.

"Wateule watatu wa tuzo hiyo walikusanywa, kwa ushirikiano na wadau wake wa soka, na orodha fupi zilizoamuliwa na paneli mbili tofauti za wachezaji na makocha wa zamani," Fifa ilisema.

Mshindi wa tuzo hiyo alipigiwa kura kati ya waandishi wa habari, mashabiki, manahodha wa timu za taifa na makocha.

Tuzo hiyo ni taji la tatu la Fifa - tuzo yake ya kwanza mwaka 2019 na ya pili mwaka jana. Pia ameshinda tuzo nane za rekodi za Ballon d'Or.

Haaland alijiunga na City akitokea Borussia Dortmund mnamo Juni 2022 na kuisaidia klabu hiyo kutwaa mataji matatu ya kihistoria katika msimu wake wa kwanza, ambapo alifunga mabao 52 katika mechi 53 za mashindano yote, yakiwamo mabao 36 kwenye Ligi Kuu Englabd kwa msimu mmoja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amekuwa na msimu kama huo msimu huu, akiwa amefunga mabao 19 katika michezo 22 katika mashindano yote.

Mbappe alicheza na Messi katika Klabu ya PSG mwishoni mwa msimu uliopita, na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa alichagua kusalia katika klabu hiyo, ambapo anaendelea kuongoza orodha ya wafungaji mabao katika Ligue 1, ingawa anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu mkataba wake utakapofikia mwisho.

**Orodha kamili ya tuzo za wanaume**

**Tuzo ya Puskas:** Guilherme Madruga (Botafogo-SP)

**Tuzo ya Fifa Fair Play:** Brazil

**Tuzo ya mashabiki wa Fifa:** Hugo Miguel Iniguez

**Kocha bora wa mwaka:** Pep Guardiola

**Golikipa bora wa mwaka:** Ederson (Man City)

**Kikosi bora:**

**Kipa:** Thibaut Courtois (Real Madrid).

**Ulinzi:** John Stones (Man City), Kyle Walker (Man City), Ruben Dias (Man City).

**Kiungo:** Bernardo Silva (Man City), Jude Bellingham (Real Madrid), Kevin De Bruyne (Man City)

**Washambuliaji:** Erling Haaland (Man City), Kylian Mbappe (PSG), Lionel Messi (Inter Miami), Vinicius Júnior (Real Madrid)

## HABARI MICHEZO



# SENEGAL YATUMA SALAMU NZITO AFCON

**ABIDJAN,** Ivory Coast

MABINGWA Watetezi, Senegal wameanza kampeni yao ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), kwa ushindi mnono dhidi ya Gambia iliyomaliza na wachezaji 10.

Pape Gueye alianza kuwapatia Simba wa Teranga mwanzo mzuri, akifunga bao kwa pasi ya Sadio Mane dakika ya nne akiwa ndani ya eneo la hatari.

Kiungo wa kati wa Cardiff City, Ebou Adams wa Gambia alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kosa la kugonga mpira kabla ya muda wa mapumziko.

Lamine Camara alifunga bao la pili la Senegal baada ya kipindi cha mapumziko.

Huku Cameroon wakibanwa na Guinea iliyokuwa na wachezaji katika mechi nyingine ya Kundi C Jumatatu, ushindi wa nne wa Senegal kati ya mechi tano mfululizo bila kupoteza ulikipa kikosi cha kocha Aliou Cisse udhibiti wa mapema wa kundi hilo.

Gambia, ambayo ipo nafasi ya 126 kwenye orodha za ubora wa Fifa ni ya chini zaidi kuliko timu yoyote inayoshiriki katika michuano hiyo nchini Ivory Coast.

Gambia inanolewa na kocha wa zamani wa Yanga, Tom Saintfiet.

## Salah aiokoa Misri na aibu

**ABIDJAN,** Ivory Coast

MKWAJU wa penalti wa dakika za majeruhi wa Mohamed Salah uliiepushia Misri aibu dhidi ya Msumbiji katika mechi ya kwanza ya Kundi B kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika, usiku sana, Jumatatu.

Ushindi ulionekana kuelekea kwa Misri wakati Mostafa Mohamed alipowaweka 'Mafarao' mbele baada ya sekunde 89 pekee.

Mabao ya haraka ya kipindi cha pili kutoka kwa Witi na Clesio yaliwapa Msumbuji maarufu kama Mambas matumaini ya kuandikisha ushindi wa kwanza kabisa wa Afcon.


Lakini ndoto zao zilikatizwa wakati Domingos Macandza alipomchezea rafu Mohamed na Salah kufunga mkwaju huo wa penalti na kuipa sare Misri.

VAR ndio iliyotoa penalti hiyo baada ya mwamuzi, Dahane Beida kwenda kwenye skrini kukagua changamoto hiyo, na Salah akatulia na kupiga mpira kupitia kushoto na kutikisa nyavu ndani ya dakika ya saba ya muda wa nyongeza.

Mabingwa hao mara saba, Misri walishindwa kuonesha kiwango kikubwa katika mchezo huo, huku Salah akigusa mpira mara chache.

Mshambuliaji huyo wa Liverpool mwenye umri wa miaka 31, amezungumzia nia yake ya kushinda Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mara ya kwanza, baada ya kushindwa mara mbili katika fainali - ikiwa ni pamoja na miaka miwili iliyopita nchini Cameroon - lakini kocha mkuu Rui Vitoria anajua kwamba timu yake inapaswa kuimarika ikiwa Misri wanataka kupata taji hilo.





## *Mourinho atimuliwa AS Roma*

**ROME,** Italia

AS Roma imetangaza kwamba imewatimua kocha wake Mkuu, Jose Mourinho na wasaidizi wake katika klabu hiyo.

Mourinho alichukua mikoba ya Roma kabla ya msimu wa 2021/22 na kuwaongoza kutwaa ubingwa wa Ligi ya Europa Conference wakati wa kampeni yake ya kwanza, huku wakimaliza kama washindi wa pili mbele ya Sevilla kwenye Ligi ya Europa msimu uliopita, baada ya kupoteza fainali kwa mikwaju ya penalti.

Lakini baada ya kipindi kibaya cha kwanza msimu wa 2023/24, ambacho kimewafanya wabaki nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Serie A baada ya mechi 20, Roma wameamua kuachana na Mourinho, na kuthibitisha kufukuzwa kwake katika taarifa ya jana Jumanne asubuhi.

Taarifa hiyo ilisomeka: "AS Roma inatangaza kwamba Jose Mourinho na wasaidizi wake wa kiufundi wameondoka kwenye klabu mara moja.

"Mourinho alitangazwa kama kocha 60 katika historia ya Roma mnamo Mei 2021."

Wamiliki wa Roma, Dan na Ryan Friedkin walisema: "Tunamshukuru Jose kwa niaba yetu sote AS Roma kwa ari na kujitolea kwake tangu kuwasili kwake Giallorossi.

"Siku zote tutakuwa na kumbukumbu nzuri kutoka kwake, lakini tunaamini kwamba, kwa maslahi ya klabu, mabadiliko ya haraka ni muhimu.

"Tunamtakia Jose na washirika wake kila la kheri kwa siku zijazo."

Mourinho alifikia makubaliano ya kujiunga na Roma Mei 2021, chini ya mwezi mmoja baada ya kutimuliwa na Tottenham Hotspur.

Kabla ya kuitumikia Spurs kwa mwaka mmoja na nusu, Mourinho alitumia misimu miwili na nusu akiwa na Manchester United, akishinda mataji matatu katika kampeni yake ya kwanza na kuiongoza kumaliza mwaka katika nafasi ya pili ya Ligi Kuu England.

# PRISON YAFUATA 'UBANI' WA LIGI KUU TUKUYU

Na Oliver Albert

BAADA ya mapumziko mafupi, Prisons imerejea mazoezini na jana ilianza kambi ya siku 10, Kiwira wilayani Tukuyu, kujiandaa na Ligi Kuu Bara ambayo imesimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon).

Prisons iko nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 17 baada ya kucheza michezo 14, imeshinda minne imetoka sare tano na kupoteza mitano.

**Kocha wa Prisons, Hamad Ally, alisema wameamua kuweka kambi Kiwira kwa sababu ya kupata utulivu wa kujiandaa vizuri na ligi.**

"Kwanza tumeona kuna mazingira magumu ya kutumia uwanja wetu wa nyumbani (Sokoine Mbeya) kwa sasa kwa sababu una matumizi mengi, timu nyingi zinatumia zikiwamo za vijana, daraja la kwanza na mambo ya kijamii hivyo kuna mwingiliano sana tukaona tutakosa utulivu.

"Ndio maana tukaamua kuja kujichimbia Tukuyu ingawa mwanzo tulitamani kuweka kambi ya nje ya mkoa wetu, lakini kutokana na mazingira imekuwa changamoto kwetu.

"Tumeona kwa sasa huku Mbeya kuna baridi tukisema tutoke na kuweka kambi mikoa mingine ambayo kwa sasa ina joto ingetupa shida," alisema Ally.

Akizungumzia usajili wa timu hiyo kwenye dirisha dogo, Ally alisema ameamua kuongeza wachezaji wengi wa nafasi ya ushambuliaji kwa sababu anataka mabao.

Prisons imeongeza wachezaji sita kwenye dirisha dogo, lakini washambuliaji wakiwa wengi zaidi. Imewasajili washambuliaji Tariq Simba, George Sangija (Geita Gold) Abdulkarim Segeja (Copco), Jacob Benedictor (Mbeya Kwanza), Ally Msengi (Moroka Swallows) na beki Feisal Mfuko kutoka Majimaji.

"Tumeona eneo la ushambuliaji ndio linahitajika kuongeza nguvu kubwa zaidi kwa sababu tunataka mabao mengi yatakayotupatia pointi kwenye ligi," alisema.



Kiungo mkabaji wa Senegal, Pape Gueye (kushoto), akishangilia sambamba na Iliman Ndiaye (katikati) na Kalidou Koulibaly, baada ya kuifungia timu yake bao la kuongoza dhidi ya Gambia wakati wakishinda 3-0 kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), nchini Ivory Coast juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Fainali BSS Januari 27

Na Mwandishi Wetu

FAINALI ya shindano la kusaka vipaji vya muziki Tanzania, Bongo Star Search (BSS), msimu wa 14, inatarajiwa kufanyika Januari 27, mwaka huu katika Ukumbi wa Were House jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benchmark 360, Ritha Paulsen, maarufu Madam Ritha, alisema mwaka huu BSS imekuwa ya tofauti kwa sababu wanawake ni wengi kuliko wanaume na wana vipaji.

"Washiriki sita wameingia fainali ya kusaka vipaji nchini BSS, mashabiki jitokezeni kushuhudia. Kipaji chako mtaji wako, washindi watapata zawadi.

"Mshindi wa kwanza kuondoka na Sh. milioni 20, kiwanja mita za mraba 500, mshindi wa pili atapa kiasi cha Sh. milioni tatu na mshindi wa tatu atapata kiasi cha Sh. milioni moja wengi kupata kifuta jasho," alisema.

Alisema kwa mwaka huu hawakwenda Dodoma, lakini walikwenda Kigoma, Arusha, Mwanza, Mbeya na kwingine na kwamba kulikuwa na washiriki wengi wakike wanaoimba na kufanya vizuri zaidi na kufika fainali hivyo ni msimu mzuri zaidi.

"Vijana 5,700 walishiriki katika shindano la BSS na hatimaye kubaki washiriki sita watakao chuana Januari 27 na mshindi kupatikana."

Ofisa Sanaa kutoka Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), William Makame, alisema sanaa wanayofanya BSS ya kutoa furaha kwa vijana ni kitu kikubwa na chakupongezwa kwani wanawasaidia vijana kufikia ndoto zao.

# MAJEMBE SIMBA, YANGA SC

INATOKA UK. 24

aliyetimkia Mashujaa, na Tariq Simba, aliyekwenda kujiunga na Prisons.

**IHEFU FC**

Walioingia: Manu Lobota kutoka FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Abubakar Khomeiny kutoka Singida Fountain Gate.

Walioondoka: Shabani Msala aliyetimkia Mtibwa Sugar na Charles Ilanfya, ambaye naye amejiunga na Mtibwa.

**MTIBWA SUGAR**

Walioingia: Jimmyson Mwanuke kutoka Simba, Shabani Msala (Ihefu) na Charles Ilanfya pia kutoka Ihefu.

Walioondoka: Ladack Chasambi aliyesajiliwa na Simba.

**NAMUNGO FC**

Walioingia: Meddie Kagere kutoka Singida Fountain Gate na Ayoub Semtawa aliyesajiliwa kama mchezaji huru.

Walioondoka: Shiza Kichuya aliyesajiliwa na JKT Tanzania, Reliants Lusajo aliyekwenda Mashujaa FC.

**DODOMA JIJI**

Walioingia: Anuary Jabir (Kagera Sugar), Apollo Otieno (KCB ya Kenya), Robison Kamura (Kakamega Homeboyz ya Kenya).

Waliotoka: Joseph Zziwa

**Coastal Union**

Walioingia: Chrispin Ngushi (Yanga), Salim Aiyee (Mbuni FC), Paulin Kasindi (Tabora United), Shadrick Mulungwe (Green Eagle ya Zambia).

Waliotoka: Balama Mapinduzi, Juma Mahadhi, Fran Golubic, Yakub Abdullah, Daud Mbweni, Abdulswamad Kassim, Henock Mayala, Justin Ndikumana na Djery Konare na Yakub Abdalahi Salah.

**JKT TANZANIA**

Walioingia: Shiza Kichuya, Mateo Anthony. Waliotoka: John Mwanda

**SINGIDA FOUNTAIN GATE**

Waliotoka: Meddie Kagere, Bruno Gomes, Joash Onyango, Elvis Rupia, Duke Abuya na Aboubakari Khomeini.

## Stars yasaka rekodi

INATOKA UK. 24

ma haitowaathiri sana wachezaji kwa sababu ni kama ya Dar es Salaam tu, huku akiongeza kuwa wapo kwa ajili ya kuipa sapoti Stars, lakini pia kujifunza kwa sababu 2027, Tanzania itakuwa mwenyeji wa michuano hiyo.

Stars ambayo ipo Kundi F, itacheza mechi hiyo saa mbili usiku, huku Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambazo nazo zipo kwenye kundi hilo, zikitarajiwa kucheza saa 5:00 usiku.

Mwaka 1980 ikiwa Kundi A, ilimaliza mechi zake za AFCON ikiwa imecheza mechi tatu, ikipoteza mbili na sare moja ikishika nafasi ya mwisho, na 2019 ilipotinga kwa mara ya pili ilimaliza ikiwa imepoteza mechi zote tatu ikishika nafasi ya mwisho katika Kundi C.


# Michezo

Jumatano Januari 17, 2024

Nipashe




Mourinho atimuliwa AS Roma UKURASA 22




Joseph Guede Yeison Fuentes Freddy Kouablan

# MAJEMBE SIMBA, YANGA NA USAJILI KLABU ZOTE LIGI KUU

## Fahamu nani katoka na nani kaingia dirisha dogo likifungwa juzi usiku...

**Adam Fungamwango na Oliver Albert**

DIRISHA dogo la usajili kwa klabu za Ligi Kuu, Championship na First League, lilifungwa juzi saa 6:00 usiku ambako kulikuwa na pilikapilika nyingi za viongozi kuhamisha wachezaji kutoka upande mmoja kwenda mwingine.

**Viongozi walikuwa wakihaha kukamilisha uhamisho kabla dirisha kufungwa kwa kusajili wachezaji kutoka nje na ndani ya nchi. Wapo wachezaji waliosajiliwa wakitoka kwenye klabu zao na wengine wakiwa huru, lakini kuna waliotolewa kwa mkopo.**

Kwa mujibu wa vyanzo vyetu kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), hawa ndio wachezaji waliofanikiwa kuhamishwa juzi kabla ya dirisha hilo kufungwa.

**SIMBA**

Walioingia: Babacar Sarr kama mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na Klabu ya US Monastir ya Tunisia, Salehe Karabaka kutoka JKU ya Zanzibar, Omar Jobe (Zhenis ya Kazakhstan), Freddy Michael Kouablan (Green Eagles ya Zambia) na Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar.

Walioondoka: Jimmson Mwanuke kwenda Mtibwa Sugar, Shaaban Chilunda kwenda KMC, Nassor Kapama kwenda Mtibwa Sugar, Jean Baleke ambaye amemaliza kipindi chake cha mkopo akielekea Klabu ya Goliath ya Bangladesh, Moses Phiri ambaye ameelekea Power Dynamos ya Zambia na Mohamed Mussa.

**YANGA**

Walioingia: Joseph Guede akiwa ni mchezaji huru, Augustine Okrah (Bechem FC ya Ghana) na Shekhan Ibrahim kutoka JKU ya Zanzibar.

Walioondoka: Jesus Moloko ambaye bado haijajulikana mpaka sasa klabu anayoelekea na Hafiz Konkoni ambaye anajiunga na Klabu ya Dogan Turk Birligi ya Cyprus kwa mkopo mpaka mwishoni mwa msimu.

**AZAM FC**

Walioingia: Franklin Navaro kutoka Tulua FC ya Colombia, Yeison Fuentes (Itagui FC ya Colombia) na Mohamed Mustafa kutoka El Merrikh ya Sudan ambaye yupo kwa mkopo wa miezi sita. Walioondoka: Idris Mbobo.

**MASHUJAA FC**

Walioingia: Mapinduzi Balama kutoka Coastal Union, Reliants Lusajo (Namungo FC), Emmanuel Mtumbuka (Stand United), David Ulomi (Moroka Swallows ya Afrika Kusini) na Erick Johora aliyetoka Geita Gold kwenda Namungo.. Walioondoka: Hakuna.

**PRISONS**

Walioingia: Abdulkarim Segeja kutoka Copco, Tariq Simba (Geita Gold), Ally Msengi (Stellenbosch ya Afrika Kusini), Jacob Benedict (Mbeya Kwanza) na Feisal Mkoko mchezaji huru. Walioondoka: Edwin Barua na Omari Abdallah.

**KMC FC**

Walioingia: Shaaban Chilunda akijiunga kwa mkopo kutoka Klabu ya Simba, Abdallah Lanso (Mlandege) na Akram Mhina aliyetoka KVZ. Walioondoka: Hakuna.

**GEITA GOLD FC**

Walioingia: Erick Mwijage kutoka West Armenia FC.

Walioondoka: Erick Johora

INAENDELEA UK. 23

# Stars yasaka rekodi AFCON

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars leo itakuwa na kazi moja tu kwenye Uwanja wa San Pedro nchini Ivory Coast, kujaribu kuweka rekodi ya kushinda kwa mara ya kwanza katika mechi ya makundi ya Mataifa ya Afrika (AFCON), itakapocheza dhidi ya Morocco saa mbili usiku kwa saa za Afrika Mashariki, huku Kocha Mkuu Mkuu, Adel Amrouche, akisema amewaandaa vema wachezaji wake kwa ajili ya mechi hiyo.

Stars haijawahi kushinda mechi yoyote ya fainali za AFCON mara zote mbili ambazo imefanikiwa kuingia mwaka 1980 na 2019.

Amrouche amesema wachezaji wake wako fiti kwa asilimia 99 na amewataka kuweka rekodi nzuri kwenye michuano hii zaidi ya iliyopita.

„Ni mechi ngumu, Morocco ni moja kati ya timu vigogo vya soka barani Afrika, lakini tumeona katika michuano hii timu zile zinazoonekana ndogo zikizifunga au kuwasimamisha vigogo, hivyo hakuna chochote ambacho tutahofia kucheza na timu hiyo kwa nia moja tu ya kupata ushindi," alisema kocha huyo.

Alisema anachosubiri ni muda ufike ili wachezaji wake wakakitoe kile ambacho amekuwa akiwafundisha katika uwanja wa mazoezi.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro ambaye yupo nchini humo kwa ajili ya kuisapoti Stars, amesema baada ya kuitembelea kambi pamoja na mazoezi ya mwisho alichokiona ni morali ya hali ya juu kwa wachezaji.

„Nimepata fursa ya kumsalimia kila mchezaji na kila aliyekuwapo kwenye benchi la ufundi, nilichokiona timu ipo timamu, morali ipo juu sana, hii inanipa moyo kwamba timu yetu sasa ipo tayari kupambana kwenye mashindano haya, mtaalam wa viungo ameniambia wachezaji wako fiti kuikabili Morocco na hata Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo," alisema Dk. Ndumbalo.

Naye Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, amewatoa wasiwasi Watanzania kuhusu hali ya hewa ya huko akise-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >